# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report Of

# DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, KILOME CONSTITUENCY HELD AT A.B.C ANZAI

ON

15TH OCTOBER, 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, KILOME CONSTITUENCY, HELD AT A.B.C. ANZAI ON 15TH OCTOBER, 2002**

**Present:**

Com. Abida Ali Aroni

**Secretariat in attendance:**

Collins Mukewa – Programme Officer
Susan Mutile – Verbatim Recorder
Sammy Kiteng'u – District Coordinator

The meeting started at 11.15 am with Mr. Sammy Kiteng'u calling the meeting to order. Mr. David Kilukya said the prayer.

**District Coordinator:** Wale wanafunzi wa..... those who are registering please, mkisha maliza ku-register you can come in. Let's hope that hawa wanafunzi wataingia kama tunaendelea. So I take this opportunity to welcome you to this session na nitaanza kwa kuwasalimia ....

Greetings: ( in Kikamba)

Nataka kuchukua nafasi hii tena kuwajulisha wale watu wamefika siku ya leo, na nitaomba Paster David Kilukya atuombee

tukianza mkutano wetu wa leo.

**David Kilukya:** Kabla sijaomba namsalimu kwanza. Hamjambo? Na wakalibisha hapa A.B.C Anzai na niwaambia pahali pa haja. Kuna choo viwili pale na hizi zitatumiwa na Commissioner na watu wake wale amekuja naye, kuna zingine ziko pale. Zile ziko pale mbele ni za wasichana na kuna zingine hapa zinatumiwa na wanaume. Kwa hivyo mnaweza kutumia hizi ziko hapa. Wanawake na wanaume watumie zile ziko pale. Asanteni. Hebu tuombe.

Maombi: Baba katika jina la Yesu Kristo tunasema ni asante kwa ajili wa siku ya leo. Tunasema ni asante kwa ajili ya kuongoza Commissioner na wote waliokuja pamoja na hata kuongoza wale wengine kutoka mahali mbali mbali wakaingia katika siku ya leo. Tunakuomba wakati huu ambapo tunaomba uweze kuwa pamoja nasi. Tunaomba ili ukaweze kutupatia mawazo, na maono ambayo inaweza kutusaidia tukajenga constitution yetu na hata kusaidia kurekebisha katika constitution ile tuko nayo Baba tukiona tumemaliza tutakushukuru na tutasema ni Asante. Tunaomba hata kwa wale wako njiani Baba ukaweze kuwasaidia na ukaweze kuwasaidia na wakifika tuendelee pamoja tutakushukuru. Wakati wote tutakao kaa mahali hapa tunaomba baraka zako, tunaomba ufunuo wa Roho wako mtakatifu, ukaweze kutupatia maneno na maono ambayo inastahili kwa ajili ya nchi yetu na kwa ajili ya mwananchi, Bwana tutakushukuru na tunasema ni asante. Ukasaidie Commissioner na ukasaidie sisi wote kwa kusema ile inastahili itasaidia kujenga Constitution yetu. Baba ukatumbaliki kwa kila jambo. Tumeomba hayo yote na tunaamini ni katika jina la Yesu Kristo aliye Mwokozi wetu. Amina.

**District Coordinator**: Asante sana Pastor Kilukya. Nilikuwa nimewambia nitawambia majina ya wale wamesaidia kufanikisha siku ya leo, nao wanaitwa 3C's nitawaomba as I call their names wanasimama wana just wave ndiyo muwaone. Nitaanza na Mr. Joshua K. Wambua, who is the Chairman of the Committee; tuna Mr. Titus K. Maundu, Secretary of the Committee; kuna Mr. Samuel Nguava, Vice Chairman; kuna Ms. Dorcas M. Kennedy, a Member ako pale nje nafikiri mna mjua, she is recording. Na kuna wale watu walishiriki kuwafunza juu ya Katiba, that is Civic Education Providers, wale wako present tuna William N Matheka na huyo pia amechaguliwa kama one of the 3 delegates from Makueni district. Kuna Authur M. Nzomo, kuna Joseph Mutungi, na pia nimeambiwa kuna Councillor moja amekuja anaitwa John Nzioki kutoka Mokaa. Na mimi naitwa Sammy Kiteng'u na ndiyo District Coordinator wenu.

Tukiendelea nataka kuchukua nafasi hii kumkaribisha Commissioner ambaye tuko naye anaitwa Abida Ali Aroni na ni Vice Chairperson wa Prof. Yash Pal Ghai, karibu sana. Na tuanze kikao chetu cha leo.

**Com. Abida:** Asante, hamjambo? Ningetaka kumkaribisha katika kikao hiki cha leo na kueleza kwamba ni mefurahia kwa sababu tumekutana tena mara nyingine baada ya kuwa hapa na wenzangu kuchukua maoni yenu. Na kwa siku ya leo ni meandamana na Collins Mukewa ambaye ni Programme Officer atakaye kuwa akitusaidia kwa kazi hii na Susan Mutila ambaye ni Verbatim Recorder. Kwa vile saa zimeenda sana, tulikuwa tuna wasubiri ili tusianze kikao na watu wachache, nitawapeleka kupitia programme ya siku ya leo kwa haraka kidogo na kufupisha mambo ambayo nadhania munayo ajua ili

tuweze kuzungumza juu ya hii draft constitution kwa dakika nyingi zaidi.

Katika programme ya leo tunatakiwa kuzungumzia madhumuni ya mkutano wa leo. Na takiwa ni wazungumzie kuhusu malengo ya urekebishaji wa katiba. Nadhania nyote mnajua ni kwa nini Katiba inarekebishwa kwa hivyo sitazungumza jambo hilo. Halafu tunatakiwa tuangalie process ambayo tulipitia hadi kufikia wakati huu ambapo tuna draft constitution. Halafu ninatakiwa kuwapitisha kwa hiyo draft constitution na kuwapa nafasi ya kuuliza maswali ama kujadiliana ikiwa kuna mtu ana jambo la kusema. Kwanza kabisa ningependa kuwajulisha kwamba tumekuja haswa kwa kuwaletea draft constitution ingawa ninajua wengine mumesoma kupitia kwa gazette na pengine mumesikia kuhusu mambo ya draft constitution kwenye radio lakini tukaona vile kuna muda tuje hapa rasmi, ili kuzileta na kuweza kufafanua ikiwa kuna sehemu ambazo hamkuelewa, na kujibu maswali yeyote kuhusu jinsi ambavyo tuliweza kuandika hii draft constitution.

Wakati tulikuwa hapa miezi kadhaa iliyopita kuchukua maoni, tuliwaelezea kwamba tutarudi kwenye province ili kuweza kuwapatia nafasi ya kusoma repoti na kujadiliana zaidi. Lakini kwa sababu ya haraka iliyoko kwa upande wa kumaliza hii katiba, bunge ilibadilisha sheria mwezi uliopita ikawa sasa hakuna lazima kuja katika province. Lakini kama Tume tukaona tuna muda tangu tulitoa hii draft hadi wakati wa National Conference tarehe ishirini na nane wa mwezi huu, tukaona ni vizuri kutumia wakati huu kuja na kuzungumza na nyinyi ndiyo mpate kuelewa zaidi. Na pengine kuna mambo mtataka kujua ni kwa nini, tuliandika hivyo, tuwaelezee na muweze kuwapatia instructions delegates ambao ni watatu mtakao kuwa mmewatuma in the National Conference pahali ambapo tutawaidhinisha au kubadilisha, hii Katiba ili hatimaye tupate Katiba ambayo itapitishwa bunge na iwe ndiyo lasmi ya nchi yetu.

Sasa hayo ndiyo madhumuni ya kwetu kufika na ningependa kuwaelezea kwa kifupi sana kwamba baada ya kuchukua maoni yenu, na tukatembea kote nchini na katika constituencies zote 210 za nchi yetu ili kuchukua maoni tuliweza kuwa na watu katika commission ambao waliweza kuchambua maoni yenu. Na kwa upande wetu kama Tume tuliweza mbali na kuangalia maoni yenu tulizungumza na wataalamu tofauti, wataalamu wa mambo tofauti tofauti ambao ni wananchi wa Kenya na pia tukapata wageni ambao waliketi na tukazungumza na wao tukajadiliana ili tupate maarifa zaidi na hapo tukaangalia maoni yenu na tukaangalia mambo ambayo tuliketi katika workshop tofauti na kuweza kutoa repoti ambayo tunaiita “the people’s choice” repoti ambayo imeangalia maoni ya wananchi ambayo yamechabuliwa na pia imetoa mwelekeo kulingana na mambo mbayo tulijadiliana na hatimaye ikatuweshesha kufanya mjadala ikiwa tuko kama Tume na kuweza kutoa hii draft constitution kupitia hizo background papers tulizozitoa, na pia maoni yenu.

Bw. Coordinator pengine ataweza kuwapatia repoti fupi a short version ya report ambayo tuliandika kabla hatujaweza ku-debate na kutoa hii draft constitution na report halisi bado inatengezwa kulingana na muda ambao tulikuwa nao hatukuweza kugojea mpaka hiyo report ichapishwe na itoke. Ndiyo tukaona itakuwa ni rahisi kutoa short version ambayo mtaweza kusoma kwa haraka kwa sababu ile nyingine itakuwa labda ni kitu kinafaa kuwa kwenye library. Sasa ndiyo tukatoa toleo fupi la report ambayo tulichapisha kwenye gazettee pia na kama nilivyo sema mtaweza kupata copy pengine hazitatosha lakini tumembeba

copy kadhaa ambazo mtaweza kusoma na zingine tutaweka katika documentation centre muweze kufika kule na kuangalia.

Na kwa sababu pengine mmesoma kwenye magazette matamshi ya kisiasa bila kuyataja ningependa kuwaambia kwamba katika Tume kabla hatujaamua jambo tuna njia tatu ambazo tunatumia kwa kubaliana ama kwa kuweza kutoa oni lolote. Kwanza kabisa tunafuata sheria ambayo ilitunga tume hii na imetupa njia tatu ya kuweza kufikia matoleo ya shughuri zetu.

Kwanza kabisa huwa tunakubaliana kwa kauli moja. Yaani kuna kuwa jambo likitokea kila mtu anasema haya sawa sisi sote tunakubaliana na jambo hilo. Ikiwa hatukukubaliana tunajadiliana na tunaangalia consensus. Kuangalia ni watu wangapi ambao wanamsimama mmoja.

Ikiwa ni watu wengi na hakuna tashwishi tuseme hata ukitupa macho unaona karibu kila mtu amekubali sasa tunatoa hiyo kauli moja kupitia consensus. Ikiwa ni vingumu kutambua, tunapiga kura. Na tukipitia juu ya hizo tatu na kuwa neno hilo ama jambo likitoka linakuwa ni jambo ambalo ni la Commission na Tume bila tashwishwi. Kwa hivyo wakati ambapo tulikuwa tunaandika hii draft constitution hakukutokea nafasi ya kupiga kura, mara kwa mara watu walikubaliana kwa wingi lakini mara nyingi mambo mengi yalikubalianwa kwa kupitia consensus. Kwa hivyo niliona niwambie hivyo kwa sababu kuna matamshi yamewekwe kwenye gazette kwamba watume ni hivi na vile, nilikuwa nataka kuwaeleza hiyo ni propaganda na jambo hili mambo yale yako mengi hayakukubaliana 100% lakini yalikubaliwa kupitia consensus na sheria ambayo imeunda tume.

Sasa kwa hayo nadhania ingekuwa ni bora tukiweza kutazama hii draft constitution. Ningewaomba wale ambao ni wasomi wa haraka haraka wanaweza kupitia kwa wengine pengine msikize lakini nitakuwa nafanya reference kwa section tofauti na jambo ambalo nimesahau kuwaambia ni kwamba a draft constitution mswaada ulitoka Jumapili kwamba gazette la taifa leo na ninadhania kuna zingine ofisini sisi tuliondoka kwenye ofisi, hii ni wiki yetu ya pili na hatukuweza kurudi kuchukua kwa sababu shughuri zetu nyingi sasa tumeziendesha upande huu wa Eastern, lakini nina hakika Bw. Coordinator ataweza kuwaletea hizo copies za Kiswahili kwa watu ambao hawaelewi lugha ya Kiingereza ili msome na kuzindi kuelewa. Na pia hiyo report mnaweza kupata zingine haziko kwa lugha ya Kiswahili lakini sidhanii ni leo anaweza kuleta hizo baadaye na ni kwa sababu kwa kawaida wasomi huwa wanafikiria kwa Kiingereza halafu wakatafusiri kwa Kiswahili. Kwa hivyo nakara nyingi zilitokea kwa Kiingereza halafu ndio zikatafsiriwa kwa Kiswahili. Na pia tukaona tukizingojea tutakuwa tumepoteza muda na muda sio mrefu nafikiria sasa tumembakisha wiki moja unusu kabla ya National Conference au kikao cha Kitaifa, tukaona tuzungumze na wanaoelewa Kizungu wataelemisha wengine kabla hamjatoa toleo liliotolewa kwa Kiswahili.

Sasa tulipofika hapa kwenu nakumbuka wengi mulituambia kwamba kuna haja ya kuwa na Utangulizi katika Katiba kwa sababu ya Katiba yetu ya wakati huu, haina utangulizi wala mwelekeo wa kutuonyesha ni Katiba ya kuongoza akina nani. Na mkatoa mapendekezo mengi kuhusu preamble au utangulizi, wengi mkasema mnataka wananchi watambulike, mkasema mnataka tumtambue Mungu, mkasema mnataka walio pigania uhuru na mambo kama hayo.

Sasa katika ukurasa wa kwanza tumechapisha proposed preamble, samahani ukurasa wa pili, nadhania iko hapo watu ambao wameangalia angalia wameona katika ukurasa wa pili na iko na chapa kubwa imeandikwa preamble, tumeweza kupendekeza utangulizi ambao unaanza kwa kututambua sisi kama Wakenya na kutambua kwamba Katiba hii ni Katiba yetu kama wananchi. Tumeangalia na kupendekeza katika utangulizi huo kwamba tunatambua utofauti wetu wa kidini, kimira, na za kikabila. Na hata ingawa kuna tofauti hizo tumejishughulisha na kujalibu sana kuishi na amani na umoja. Pia tumependekeza kwamba tutambue umuhimu wa watu binafsi, familia na jamii hapa nchini. Tumependekeza kwamba tutambue jitihada ambazo zimetendea na wanawake na wanaume kwa kuweza kuleta serikali ambayo inafaa ama utawala ambao unafaa ambao ni wa demokrasia na unatambua uhuru wa kila mwananchi na serikali ambayo itaendeshwa kupitia sheria za nchi.

Pia tumetambua kwamba sisi kama wananchi tumejishughurisha na juhudi za kurekebisha Katiba ili tuweze kujumuika katika utawala wa nchi yetu na hapo mwisho tumetambua Mwenyezi Mungu. Sasa hii preamble ambayo tumependekeza mtaweza kuangalia na kuona kwamba ina kasoro na pengine kuna mtu ambaye ana mambo zaidi ambayo yangefaa kuwekwa katika hii Katiba.

Katika chapter ya kwanza, tumeangalia ukuu wa mwananchi wa kawaida. Katika article ya kwanza au ukurasa wa kwanza tumependekeza kwamba sisi kama wananchi ndiyo watu ambao tuna nguvu na tunawapa nguvu hizi watu ambao wanatutawala. Na tumependekeza kwamba nguvu hizi ambazo tumewapa watu hawa au mamlaka ambayo tumewapa itumike kwa njia ya kidemokrasia. Na tukasema kwamba mamlaka ya utawala tumeyatoa kwanza kabisa kwa bunge ambapo tumetuma wakilishi wetu pale ili wafanye shughuli zetu kulingana na Katiba hii.

Halafu mamlaka ya pili tumeyatoa kwa serikali kuu ambayo pia tunayatarajia itaongoza nchi kwa kupitia mambo ambayo ni ya kikatiba.

Tatu, tumetoa mamlaka kwa mahakama ili iweze kutoa hukumu ambazo ni sawa kulingana na Katiba hii.

Nne, tumetoa mamlaka kwa vyombo ambavyo ni vya kikatiba ambavyo mmeona tumependekeza katika chapter ya kumi na saba ili kujihusisha na kusaidia serikali katika utawala wa nchi.

Katika ukurasa wa pili tumeangalia umuhimu wa Katiba na tukaeleza kwamba Katiba ndiyo itakayokuwa na uongozo katika sheria kuu ya nchi na kwamba Katiba hii ni lazima izingatiwe na watu wowote wako mamlaka. Na kwamba ikiwa kuna sheria yoyote ambayo hayabatani ni hii Katiba sheria hiyo basi itakuwa haifai kutumiwa na itakuwa ni lazima iondoshwe.

Na tukapendekeza jinsi Katiba hii itatumika. Tumependekeza kwamba Katiba hii itumiwe kwa kuweza kueneza maadili ambao yanafaa katika uongozi bora. Tumependekeza kwamba Katiba hii ifuatwe katika kueneza haki za kibinadamu, haki za kimsingi,

uhuru wa mwananchi na pia sheria katika utawala, na tumependekeza kwamba sheria hii pia itumike na ihusishe maendelea katika nchi.

Katika article ya tatu, tumependekeza jinsi ambavyo tutahakikisha kwamba Katiba yetu itaweza kutekelezwa na tumependekeza kwamba mtu yeyote aweza kuenda katika mahakama ili kushtaki kwa jambo lolote ambalo limekosa kutimizwa kwa kufuata Katiba hii.

Halafu tumetazama sheria zingine za nchi katika article ya tano na tumependekeza kwamba tuwe na sheria kadhaa. Tumependekeza Katiba kama sheria kuu ambayo itafuatiwa na sheria zinazotungwa ama kutengezwa na parliament. Tumependekeza pia sheria za kitamaduni. Tulipokuwa hapa mlilalamika na kusema sheria za Kakamba zimetupiliwa mbali na tukapendekeza kwamba pengine tukipendekeza sheria hizo mambo yatabadilika na kuwa ni mazuri. Tuliambiwa hivyo na wananchi wengi mnapendekeza kwamba kwa hii sheria mpya sheria zetu za kitamaduni ziwe zinapewa nguvu. Tumependekeza kwamba sheria ya jamii ya Waislamu na Wahindu pia itambuliwe. Tumependekeza tena pia kwamba mambo ambayo yametendeka kwa miaka mingi na hatimaye yakawa ni kama sheria mambo ambayo kwa sheria tunaita common law yatumike pia kama sheria. Tumependekeza pia kwamba sheria zitakazotungwa na jumia ya Africa mashariki ziweze kutumika hapa nchi. Hatutaki sheria zitungwe kwenye mikutano ya Africa mashariki lakini tukifika Kenya tunazitupa ama kuchagua kwa sababu zingine haziwapendi watawala wetu.

Pia, tunapendekeza kwamba mikatamba ambayo yanawekwa sahihi na serikali katika mikutano ya kitaifa, international law yaweze pia kutumika hapa nchini. Kwa wakati huu hakuna sheria inayolazimisha mambo kama hayo na unaona kwamba tume tia sahihi mikataba mingi ya kitaifa lakini kwa sababu pengine mikataba hiyo tunaona haifai utawala wanazitupilia mbali. Sasa tunapendekeza kwamba ni lazima tukiweka sahihi mikataba ya kitaifa itengezwe kuwa ni sheria tutakapofika hapa nchini.

Chapter ya pili tunaangalia Jamhuri ya Kenya na jinsi ambavyo tutaendesha utawala katika nchi hii. Tumependekeza kwamba Kenya iwe ni demokrasia ya vyama vingi. Tumependekeza pia Kenya iwahusishe wananchi wa kawaida katika utawala na kwamba kuwa na uwazi na uwajibikaji wa utawala wa wananchi ambako tutakuwa na hivi vyombo tofauti vya kiserikali tukipewa nafasi ya kufanya kazi yake na pia kuwe na uhuru, haki za kibinadamu, na pia tuwe tuna zingatia sheria.

Tumeangalia pia mipaka tofauti ya nchi yetu na katika kurasa za nyuma na hii nakala ambayo mnayo tumeweza kutoa mipaka ya nchi jirani na Kenya. Kwa mfano ukiangalia schedule ya kwanza kule nyuma mtaona tumeeleza kwa kirefu mipaka yetu na Uganda, Tanzania, Sudan, Ethiopia na Somalia. Mkiangalia schedule za nyuma baadaye nafikiri kwa ukurasa kuanzia thelathini na tisa kuenda mbele mtaweza kusoma baadaye muone tumeweka mipaka ya nchi yetu.

Pia tumeangalia lugha ambazo zitatumika na tumependekeza katika article ya tisa kwamba Kiswahili na Kiingereza zitumike kama lugha ambazo ni rasmi official languages. Kwa wakati huu lugha rasmi ni Kiingereza simanelewa hivyo? Sasa ukienda

kwa mahakama na Judge ni Mkamba, interpreter ni Mkamba, Judge anataka uongee na Kizungu, si ni ukweli? Ama ukiongea na Kikamba interpreter ana tafsiri kwa sababu sheria imesema official language, na tukaona mambo hayo hayafai. Na tukapendekeza pia Kiswahili, kiendelee kuwa lugha ya kitaifa lakini serikali itambue lugha zote za nchi yetu za makabila tofauti na kukuuza lugha hiyo ili tuweze kuzidi kukuuza utamaduni wetu. Tumependekeza pia mbali na lugha za kitaifa, serikali ikuuze lugha ya ishara, sign language ambayo inatumika na watu ambao ni walemavu na pia ikuuze drill kwa sababu hiyo ndiyo lugha ambayo inaeleweka na watu ambao ni vipofu.

Tukaangalia serikali na dini katika article ya kumi na tukasema kuwe na mgawanyiko wa dini na serikali lakini hatukusema kwamba watu ambao ni viongozi wa dini wasijihusishe na siasa. Muangalie tunasema, state and religion. Serikali na dini zitofautishwe. Na kuumanisha hivyo tumeendelea na kusema au kupendekeza kwamba serikali iwe ni secular sio serikali ya kidini. Na sababu ni kwamba tuna madhehebu mengi, dini tofauti hapa nchini na hatukutaka kupendekeza, dini hii au dhehebu hii kupinga zingine, na tukasema kwamba dini zote zipewe usito sawa katika shughuri za kiserikali.

Ukurasa wa kumi na saba tumependekeza national symbols au vyombo ambavyo vingine ni vya kitaifa. Tumependekeza bendera ya Kenya, wimbo wa taifa tumependekeza court of arms, au alama inayotumika kwa vitu au vifaa ambavyo ni mali ya umma na pia tukapendekeza mhuri wa serikali au public seal kuwa pia ni national symbol. Halafu pia ukurasa, kuna mambo ingine nitakuwa na ruka kwa mfano kurasa 12 inaongea kuhusu viapo vitakavyotumiwa na wafanyi kazi wa serikali na tumevitambua viapo hivyo katika schedule ya nne mtaangalia baadaye.

Pia tumependekeza siku za kitaifa na tumependekeza siku tatu. Tumependekeza tarehe mosi mwezi wa June ambayo inajulikana kama Madaraka day, tumependekeza tarehe kumi na mbili December, Jamhuri Day na tukapendekeza kwamba tuwe na siku ya Katiba. Sasa mtaangalia muone kwamba kama hayo mapendekezo yanafaa ama mna mambo mengine zaidi yakuongezea.

Katika chapter ya tatu, tumeangalia madhili au misimamo ya kitaifa, National Values and Goals. Na tukasema kwa sababu wananchi wengi walisema nchi yetu haina misimamo rasmi na kila serikali kawaida inakuja na misimamo yake pengine kuna haja yakuandika values na goals ili tujue kwa kila wakati nchi hii ina msimamo ya aina gani. Na tumependekeza values karibu kumi na nane lakini kwa kifupi sana nitawasomea mambo ambayo tumependekeza.

Tumependekeza uhuru wa wananchi, umoja wa kitaifa, usawa na tudhamini jamii zote kwa usawa, tuwe na demokrasia na utawala mwema na utawala unaozingatia sheria. Tumependekeza kwamba utawala wetu uzingatie haki za kibinadamu, haki na usawa bila kubagua mtu kwa sababu ya jinsia yake, kuwa na bidii ili kuweza kupata mafanikio yatakayo tupatia mahitaji ya kimsingi, tuwe na kushiriki na uwazi katika shuguri za umma, uadhirifu wa kibinafsi na wa kitaifa, tuwe na uvumilivu na heshima ya maoni kwa watu wote, kukuuza mila na maadiri tofauti ya watu tofauti hapa nchini, kuwe na utawala ulio karibu na wananchi, utatuzi wa mabishano kwa njia ya amani wakati ambapo tunakuwa na mizozo tofauti na pia tumependekeza haja ya sisi

kukuuza utaifa ya nchi za Africa. Sasa hayo ni baina ya mambo ambayo tumependekeza lakini mtaweza kusoma kwa kirefu baadaye.

Pia tumeangalia baada ya kusema goals and principles ambazo ni mewasomea ambazo nyingi pengine zitatakiwa kutekelezwa na serikali, tumeangalia je, kuna majukumu ya wananchi na kwa katiba yetu ya wakati huu mwananchi hajaandikiwa majukumu yake na unakuta mala kwa mara sisi kama wananchi huwa tunasema serikali haijatufanyia hii, serikali haitupatii maji, serikali haitengezi bara bara, lakini hatuangalii je na sisi tuna jukumu gani la kuhakisha kuna mabarabara, kuna madawa na mambo kama hayo. Tukaona itakuwa ni vizuri tuandike ili sisi kama wananchi tunjue majukumu yetu ni nini.

Na kwanza kabisa tumependekeza kwamba ikiwa tunataka kuwa na maadili au misimamo ambayo yataweza kutusaidia kama wananchi ni lazima sisi sote tuwe na majukumu yanayofuata. Kwanza kabisa tuweze kusoma Katiba ya nchi yetu ili tuweze kuieneza na kuweza kuzingatia mambo ambayo yako pale, na pia ni lazima sisi kama wananchi tuweze kusimama imara na kuweza kutetea haki zilizowekwa katika Katiba.

Tatu ni jukumu letu kama wananchi kuweza kuzingatia mambo ya kidemokrasia kama vile upigaji wa kura nakujihusisha na siasa za nchi. Mfano mzuri ni hivi: kawaida kama Kilome Constituency, sijui mko na watu wangapi ambao mmenjiandikisha kupiga kura pengine wakaaji wa hapa ni laki moja. Utakuta pengine watu elfu hamsini wamejiandikisha kupiga kura halafu siku ya kura elfu ishirini watajitokesha. Kiongozi akitoka mnasema ah huyu hatumpendi, hatukumchagua tuliwekewa. Wengi wenu hamkati kura, wengi wenu hamjihusishi na viama vya kisiasa, lakini mnateta tuna viongozi wabaya. Hao viongozi si ni watumishi wetu? Ikiwa hatukuweka viongozi wazuri tutalaumu nani? Si ni sisi? Au tukitoa sukari na kuweka viongozi ambao hawana maendeleo, si ni sisi tunafaa kujiraumu? Sasa tunasema ni haki yetu kujihushisha na demokrasia kwa kupiga kura na pia kujihusisha na vyama vya kisiasa na siasa za nchi.

Pia tumependekeza kwamba kila mwananchi ajihushishe na kazi ama shuguli za kimaendeleo na pia ajihusishe kwa kujenga jamii, familia yake na jamii kwa jumla, kwa sababu ukiweza kutumikia familia yako na jamii utakuwa unachangia katika kukuuza uchumi wa nchi na kwamba kila mwananchi aweze kukuuza mambo anayojua kwa kazi kuongeza elimu yake ili kuchangia katika maendeleo ya nchi.

Tumependekeza pia kwamba ni jukumu la kila mwananchi kujihushisha na kuendesha jamii inayotoka na pia ni jukumu letu kama wananchi kuweza kukuuza umoja na amani ya nchi yetu ku kuuza demokrasia, pia kuweza kuchunga mali ya umma na kuhakikisha kwamba mali hii ina tumika kwa njia iliyo sawa bila kupoteza na pia kuchunga mali yetu na kuungana na kushilikiana ili kuchunga sheria, na kutojihushisha na ufisadi ama mambo ya corruption na hatimaye kuhakikisha kwamba tumeipatia nchi yetu sifa itakayotupatia nafasi katika nchi za kitaifa. Sasa hayo ndiyo tumependekeza kama majukumu yetu kama wananchi wa Kenya.

Chapter ya nne tumeangalia uraia, na tukapendekeza aina tatu za uraia, kuzaliwa, kujiandikisha na pia naturalization. Na tukapendekeza kwamba Mkenya yeyote atakayezaliwa na mama, ama mtoto yeyote atakayezalia na mama ama baba ambaye ni Mkenya atambuliwe kuwa ni Mkenya ambayo ni tofauti na Katiba ya wakati huu.

Pia tumependekeza kwamba, mtu yeyote ambaye ni raia kupitia chapter hii hawezi kunyang'anywa uraia wake kwa njia yeyote ile na tukapendekeza pia watoto wote ambao wako na umri wa miaka nane na wazazi wao hawatambuliki kuwa ni Wakenya au sio Wakenya wapatiwe uraia wa Kenya wakipatikana. Pia tumependekeza ya kwamba wananchi wa Kenya waweze kuwa na uraia zaidi ya umoja – dual citizenship. Na tukapendekeza pia kwamba itoe miongozo itakayosidia katika kufanya shuguli ambazo ni za kiraia na kuwe na board itakayowekwa kuchunguza watu ambao wanaomba kuwa raia wa Kenya.

Chapter ya tano ambayo ni muhimu zaidi, tunaangalia haki za kimsingi, fundamental rights na freedom, na tumependekeza kwa kifupi kwamba haki hizi ni za kila mwananchi na sio haki ambazo tunapewa na serikali lakini ni haki ambazo tunazaliwa nazo. Na tukatoa majukumu ya serikali kwa kuhakisha kwamba kila mwananchi anaweza kuwa na hizi haki za kimsingi. Tumependekeza kwamba serikali iweze kuheshimu na kutekeleza uajibu wake ili kuhakikisha kwamba kila mwananchi anaweza kupata hizi haki ambazo ni za kimsingi. Na pia tumependekeza katika article ya 31, kwamba wakati mwingine ingawa tumepatiwa hizi haki za kimsingi kuna weza kuwa na haja ya kuzipunguza kwa sababu kuna watu wengine hupita mipaka ukikosa kuwapatia kiwango cha jambo kama hilo.

Na tukapendekeza katika article ya thelathini na mbili kwamba kila mwananchi ana haki ya kuishi, na kwa sababu ya pendekezo hilo tukapendekeza kwamba hukumu ya kifo itupiliwe mbali kwa sababu huwezi sema kila mtu ana haki ya kuishi halafu tuna hukumu wengine kuwapatia hukumu ya kifo. Tumependekeza usawa wa kila Mkenya katika kuweza kupata hizi haki za kimsingi. Kusiwe na umbaguzi wowote kupitia rangi ya mtu, maubira yake, awe ni mwanamke, mwanaume, au kulingana na kama ameoa au ameolewa, kusiwe na ubaguzi kupitia ukabila, miaka, hali ya ulemavu, dini, lugha ama alivyo zaliwa Mkenya yeyote.

Halafu katika ukurasa wa thelathini na tano tumeangalia haki za akina mama, tuliweka haki za akina mama tofauti na hizi zingine kwa sababu akina mama wote walilalamika na kusema kwamba ingekuwa katiba imechunga haki zao hawangenyanyaswa kwa sababu wanadai kwamba kwa miaka mingi wamenyanyaswa. Na tukapendekeza kwamba akina mama wepewe haki sawa na wanaume, hasa kwa upande wa siasa, uchumi na katika jamii.

Tumependekeza pia kwamba akina mama wapewe heshima, tumependekeza kwamba waweze kupewa haki ya urithi sawa na wanaume na waweze kumiliki na kuweza kujihusisha na mali. Tumependekeza kwamba ikiwa kuna sheria yeyote au utamaduni wa aina yeyote ambayo itakosa kuzingatia haki za akina mama na kuweza kuwambagua sisi tumiwe. Tumependekeza pia kwamba serikali iweze kuchunga akina mama na kutambua sehemu yao ya kizazi katika jamii na kuwapatia nafasi ili waweze kunjijenga katika shuguli zao.

Pia tumeangalia haki za watu wazima, older members of the society ambazo tuliombwa sana kuziweka katika Katiba na ambazo haziko kwa katiba wakati huu na tukapendekeza mambo yafuatao, kwamba wazee hawa wapewe haki ya kujumuika na Wakenya wengine katika hali za kitaifa, na wepewe nafasi za kuweza kujikuza katika maendeleo wapewe haki mbila ya kunyanyaswa, kuonewa wala kutukanwa, wapewe haki zitakazowesheza kuishi kwa njia inayofaa na kwamba serikali na jamii zao ziwapatie, usaidizi unaofaa.

Tukaangalia haki za watoto pia watoto wamelalamika na kusema haki zao haziko katika Katiba na wanaonewa sana. Sasa tukapendekeza yafuatao na pia jambo hili la watoto na la wamama ni kuzingatia kama niliwaeleza mikatamba ya kimataifa. Na upande wa watoto tumependekeza kwa kifupi kwamba iwe ni jukumu kwanza kabisa la wazazi, la familia, jukumu pia la society au community kuweza kuchunga watoto hawa, kuwashomesha, kuwapatia mazingara yanayostahili kuwapatia mapenzi, na kuhakikisha kwamba watakuwa wakiwa ni watu ambao wataweza kutumika na kuwa ni watu wanaofaa katika jamii. Tukapendekeza kwamba watoto wanaozaliwa nje ya doa na wale wanazaliwa kwenye doa wasimbaguliwe katika kupatiwa haki zao za kisheria. Tupendekeza kwamba ikiwa kuna jambo lolote linalomhusu mtoto tuangalie kwanza masilahi ya huyo mtoto kabla hatujatoa uamzi. Tukapendekeza pia kwamba wazazi wote wawili mama na baba ikiwa wameoana ama wemetengana, au hawakuoana wawe na majukumu sawa katika kuwalea na kumlinda yule mtoto. Tumependekeza pia kwamba kila mtoto anastahili kupewa jina na uraia. **End of tape 1A**.

Tumependekeza pia kwamba watoto wapate elimu ya bure wa msingi na elimu hii iwe ni ya lazima, kwamba watoto wasiweze kubaguliwa wala kufanyiwa mambo ambayo hata ikiwa ni ya kitamaduni ambayo yanaweza kuwadhuru. Pia tukapendekeza kwamba watoto wasifanyishwe kazi au mambo ambayo inaweza kuwa ni ya hatari na waweze kupewa malezi ambayo ni ya kimusingi kwa mfano waweze kupata matibabu, waweze kupata mahali ya kulala na waweze kupata mambo mengine ambayo ni muhimu katika jamii.

Tumependekeza pia kwamba watoto wasiadhibiwe adhabu ambazo hazifaii, ambazo ni adhabu za kinyama na hazifai kufanyiwa binadamu iwe ni katika shule ama sehemu zingine za elimu. Na kwamba kukiwa na vita watoto wasitumike katika hali ya hatari, wasifungiwe katika magereza ila ikiwa ina lazimika na kwamba ni kwa faida na manufaa ya huyu mtoto na afungwe kwa wakati mfupi iwezekanavyo. Na wakiwekwa katika magereza ama katika cell asiwekwe na watu wazima na apewe wakili atakaemsaidia haraka iwezekanavyo na kesi yake isikizwe kwa muda mfupi.

Tumeangalia pia na kupendekeza mambo yaliyo muhimu kwa familia na jambo ambalo nitaliangalia ni kwamba kila Mkenya ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na minane ana haki ya kuoa ama kuolewa na kuunda familia. Na kwamba katika ndoa na baada ya watu hawa kutengana wana haki sawa. Mmeelewa wazee? Nataka muelewe ili muweze kutoa maoni kama ni sawa ama si sawa, sindiyo?

Pia ndoa ambazo ni za kitamanduni ziweze kuwepewa nafasi sawa na ndoa hizi zingine na kwamba bunge itengeze sheria

itakayowezesha ndoa hizi kutambulikana. Tumeangalia pia haki za watu walemavu na kupendekeza kwamba serikali iweze kuwapatia nafasi ya elimu inayostahili.

Tumependekeza kwamba serikali ihakikishe kwamba vyombo vyote vya usafiri, vyombo vyote ambavyo vinatumika kwa kueleza maneno na pia nyumba via serikali viwawesheshe watu walemavu kuweza kufika pale. Tumependekeza kwamba serikali kama nilivyosema ikuuze lugha ya ishara na drill na kwamba katika sheria zote ya viongozi ya serikali itolewe lugha yeyote ambayo ni ya kubagua watu walemavu. Watu walemavu pia wahushuswe kufika viwango tofauti vya utawala na pia kutungwe sheria ambazo zitawafaa. Na tukaangalia nje mtu mlemavu ni mtu wa aina gani? Tukasema ni mtu ambaye pengine maubile yake hayajakuwa kamili, tukasema ni mtu ambaye akili zake pengine hazipunguani, zimepungua, mtu ambaye haoni na mtu ambaye anakilema ama magonjwa fulani.

Halafu tukaangalia haki za kuwa na mali. Tumeangalia haki ambayo itakoshesha mwananchi yeyote kutimiwa kama mtumwa. Katika article ya arobaine na nane pengine mngetaka kuangalia sana tunaangalia haki za kuabundu na tumepanua haki hii na kupendekeza kwamba kila Mkenya apate haki ya kuabundu, kuwa na mafikira ya kidini na kuwa na maoni yeyote ya kidini. Tumependekeza pia kila Mkenya awe na haki ya kuabundu akiwa peke yake na jamii na pia anaweza kuabundu nyumbani ama katika sehemu ambayo ni ya watu wengi na kwamba akiabundu aweze kupewa nafasi ya kuamini na kuweza kufanya mambo yanatakikana katika dini yake. Na hatukusema dini ni kumcha Mungu mkisoma mtaona inasema freedom of conscience, freedom of religion, freedom of thought, freedom of belief and freedom of opinion.

Pia tumependekeza kwamba watu ambao wanasimamia vikundi via kidini wapewe nafasi ya kukuuza elimu na kunjenga sehemu ambazo zitatoa elimu. Tumependekeza pia kwamba mtu yeyote asilazimishwe kuchukua kiapo kinyume cha dini yake na pia asilazimishwe kushugulika na kukaa katika ibadda ya dini isiyo yake na asilazimishwe pia kufanya jambo lote ambalo ni kinyume na dini yake.

Tumependekeza pia freedom of expression ama uhuru wa kuweza kusema maneno. Tumependekeza pia uhuru wa kuweza kupata maneno ambayo ni ya kiserikali, tumependekeza pia tuwe na uhuru wa kuweza kuandamana ikiwa maandamamo hayo ni ya amani, haki za kisiasa kwamba kila Mkenya ana haki ya kujiunga ama kuunda chama cha kisiasa na kujishugulisha na shuguli au campaign ya chama hicho.

Tumependekeza pia haki ya kutembea na kuishi mahali pote Kenya, haki ya wafanyi biashara na walio andikwa pia tukatazama haki za wafanyi kazi. Na katika haki hizi ukurasa kumi na tano article 55 tumependekeza kwamba kila mfanyi kazi awe na haki ya kufanya kazi pahali panapostahili awe na haki ya kulipwa mshahara unaostahili, haki ya kufanya kazi masaa yanaostahili na sehemu ambayo ni sawa na kila mfanyi kazi awe na haki ya kujiunga na programme ama kikundi chochote cha wafanyi kazi na kwamba wafanyi kazi wawe na haki ya mgomo.

Halafu tumeangalia haki za waajiri, na tukapendekeza kwamba waajiri pia wawe na haki ya vyama vya waajiri na kufanya programmes zozote ambavyo vinafaa kuvifanya. Tumeangalia pia social security na tukapendekeza kwamba serikali itoe msaada kwa mtu yeyote ambaye hawezi kujisimamia na wala hawezi kusimamia familia yake. Tumeangalia pia upande wa matibabu na tukapendekeza kwamba kila Mkenya ana haki ya kupewa matibabu yanayofaa. Tumeangalia elimu na tukapendekeza kwamba kila Mkenya apate haki ya elimu ya msingi ya chini ya shule za msingi na shule ya upili na kwamba serikali itafanya mambo yote yaliyomuhimu kuhakikisha kwamba elimu ambayo ni juu ya elimu ya secondary itaweza kukuzwa ili kwamba kila Mkenya aweze kujiendelesha na kusoma.

Tumeangalia nyumba na tumependekeza kwamba kila Mkenya awe na haki ya kuishi katika nyumba inayofaa – access to adequate housing. Nyumba inayofaa sasa inategemena nafikiri mambo tofauti. Tumependekeza pia kwamba itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufukuzwa katika nyumba anayoishi mbali na kupitia mahakama na mahakama kuchunguza mambo yote yanayostahili kabla ya kutoa idhini ya kumtoa mtu katika nyumba anayoishi.

Tukaangalia chakula na tukapendekeza kwamba iwe ni haki ya kila mwananchi kutokosa kukaa na njaa. Na tukapendekeza kwamba kila Mkenya aweze kupata chakula kinacho faa na anachostahili. Tukaangalia maji na tukapendekeza kwamba ni haki ya kila Mkenya kupata maji masafi na ya kutosha. Tumeangalia mazingara na tukapendekeza kwamba ni haki yetu kuishi katika mazingara yalio mazuri masafi na yanayofaa.

Tukaangalia pia haki za ununuzi – consumer rights na tukapendekeza kwamba ni haki ya mtu yeyote anayenunua kitu ama kulipa kuweza kupata, kupewa huduma na kupewa kitu ambacho ni kizuri na kitu ambacho hakitamdhuru mtu yule na kitu ambacho kinaadamana na pesa ambazo amelipa. Na pia tukaangalia haki kutokubali kupewa amri isiyoya kisheria ama ya halali na tukasema ni haki ya kila Mkenya kutokosa kukubali amri isiyo faa.

Tukaangalia pia mahakama na tukapendekeza kwamba ni haki ya kila Mkenya kuweza kufikia mahakama kupata shuluhizo na tukaangalia haki za watu ambao wanashikwa na katika mambo yale tumependekeza ni kwamba ukishikwa una haki ya kunyamaza bila kuzungumza, una haki ya kueleza na lugha ambayo unaelewa kisababu ya wewe kushikwa na pia atakayekushika akuelezee kwamba una haki ya kunyamaza na pia unahaki ya kutoa confession ama haki ya kukili makosa na kueleza kwamba ukikili hayo makosa yanaweza kutumiwa kwa kukufunga ama kwa wewe kuadhibiwa. Na kwamba ukishikwa upelekwe kortini isizidi masaa arobaini na nane, na ukifikishwa mahakamani, mahakama ikupatie nafasi ya utetesi ulio sawa. Ikupatie nafasi iliyo sawa na utetezi wako na pia ukiwa unataka wakiri upewe nafasi ya kuchagua wakili wako. Na ikiwa kosa ambalo umeshtakiwa nalo litakuwa na adhabu ya juu serikali ikupatie wakili na pia atakaeshikwa atabuliwe kwamba hana hatia mpaka ambapo kesi yake itamalizika.

Na pia tukatoa pendekezo kuhusu watu wanaowekwa katika cells na tukasema kwamba watu hawa wanafaa kutendewa mambo ambayo yanastahili kutendewa binadamu, wapewe haki zao za kimsingi na pia wasibaguliwe, wasitendewe mambo

mabaya, na watu ambao ni wafanyi kazi wamagereza ama custody, na pia wapewe chakula kinachostahili kuliwa na binadamu. Wapewe matibabu, usafi, na nguo zinazostahili kuvaliwa na binadamu. Wapewe elimu itakayo wasaidia wakitoka jela, wapatiwe nafasi ya kuabundu, kuasiliana na jamii zao, na mawakiti wao na mengine mtazidi kusoma kwa sababu ni mengi.

Katika chapter ya sita, tumeangalia uwakilishanji wa wananchi katika bunge, the electoral system and process. Na tumependekeza kwamba kila mwananchi awe na haki ya kura na ya kusimama akitaka kusimama katika kura na kwamba kura hizi ziwe zinafanya za kisiri kwa sababu tuanona kwamba kuna wakati tulibadilisha tukasema pengine tukiweka katiba kutakuwa hakuna mabadiliko. Tukapendekeza pia kura hizi ziwe ni za haki na za halali na kwamba kura zihakikishe kwamba akina mama, watu walemavu na zilizotengwa zilihusika na upigaji wa kura. Tafadhali wanaozungumza mtupatie nafasi sisi ambao hatutaki kuzungumza tusikie maneno.

Na pia tukaangalia haki ya kupiga kura ya mwananchi na kusema kwamba mtu yeyote ambaye ana miaka kumi na nane ana haki ya kujiandikisha na kupiga kura na kwamba kuandikishwa kwa kura kuwe ni jambo linaloendelea kila wakati bila kusimamishwa. Na tukaangalia watu ambao wanaweza kujiandikisha kupiga kura na kwa kifupi Mkenya aliye na miaka kumi na minane na zaidi, mtu ambaye anaishi kwa nchi hii kwa kawaida, na mtu ambaye amekuwa anaishi kwa kawaida katika constituency ambaye anataka kupigia kura. Na tukawaonyesha disqualification ama ni kitu gani kinaweza kuzuia mtu kutoandikishwa kama mpiga kura.

Katika article ya themanini na tatu tumeangalia tume ya upigaji kura – Electoral Commission. Na tumependekeza kwamba tume hii ambayo ina watu ishirini na mbili kwa wakati huu watu hawa wapunguzwe wawe kumi na wakipungua zaidi watu nane. Kwa sababu nyinyi wenyewe mlituambia kwamba ni watu wengi na pesa ambazo zinaghalamiwa ni nyingi na kawaida hawana kazi za kufanya ingawa pia tumeongeza kazi zao, na tukapendekeza kazi zao ziwe zifuatazo.

Kwanza kuandikisha kura kwa wakati wote.

Pili kuangalia mipaka ya constituencies.

Tatu kusimimia upigaji kura.

Nne, kuweza kukuuza na kuhikisha kuna kura ya haki na ya kweli.

Tano, kusimamia na kuandikisha vyama vya kisiasa. Pia kusimamia fedha zitakazotengea kwa sababu tumependekeza fedha zitengwe vya kusaidia vyama vya kisiasa kwamba tume hii itasimamia pesa hizo. Tuumependekeza kwamba ukiwa na mizozo ya kura waweze kusimamia mizozo hiyo. Tumependekeza pia wazidi kueneza na kukuuza elimu ya upigaji kura, elimu ya demokrasia, na utamaduni na kwamba wawe wanachunga wakati ambapo kuna elections na kuhakikisha kwamba kura hizi

zinafuata njia iliyotakikana na tumependekeza kwamba tume hii iwe ni Tume huru itakayoweza kufanya kazi yake kwa kulingana na maagizo ya katiba peke yake.

Tumeeleza mambo mengi ya wafanyi kazi wa tume hiyo na jambo lingine ambalo ningependa kughusia ni article 86, inayotueleza ni nini watafanya kuhusu sehemu za uwakilishi bungeni. Na tumependekeza mambo yafuatao, kwamba watakuwa baada ya kila miaka kumi wakiangalia mipaka ya sehemu za uwakilishi bungeni na constituencies na kwamba wakiangalia mipaka hii watazungumza na kupata maoni ya wananchi. Baada ya kupata maoni wataangalia mambo yafuatayo.

Wataangalia wingi wa watu, na mahitaji yao, njia ya kuwasiliana ya sehemu hiyo, geographia ya sehemu hiyo, haja na matakwa ya jamii wanaoishi ama watu wanaoishi katika eneo hilo, mipaka ya kitawala, na pia wataangalia census itakayokuwa imechaguliwa. Kwa hivyo katika kutenga mipaka ya wakilishi bungeni tunapendekeza wasiangalie tu kuna wingi wa watu, na kusema kwamba kila constituency iwe na watu kama laki hamsini. Tunasema kuna kura kunaweza kuwa na watu wengi, kwa mfano Nairobi lakini kwa sababu ya mambo kadhaa hawawezi kuwa na constituencies nyingi. Kuna kura kuna weza kuwa na watu ishirini lakini pengine ni hardship area hawawezi kuwa na mawasiliano mazuri kwa hivyo pengine wanafaa kutengewa constituency. Sasa hivyo ndivyo tumependekeza.

Tumeangalia haki ya vyama via kisiasa na tukazungumzia kwa kirefu haki zao na tukaangalia hizi vyama vya kisiasa, kwa wakati huu sijui kama mnajua kazi yao. Mnajua kazi yao? Sasa tukapendekeza kupitia vile mlivyo tuambia kazi na majukumu ya vyama vya kisiasa. Tukapendekeza kwamba wawe wanakusanya watu na kuwaelemisha na kuwaeleza mambo ambayo ni ya muhimu katika jamhuri yetu yawe pia yanapatia watu nafasi yakuweza kujiunga na utawala, pia iweze kusomesha watu, na pia utimie uwezo wake katika sehemu tofauti za kiserikali ili kuwakilisha misimamo ya watu ama ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Na pia ihakikishe kwamba serikali itafuata mwongozo ambayo inafaa na pia ihakikishe kwamba serikali itaajibika kwa wananchi wa kawaida.

Na tukaeleza jinsi vyama hivi vitaandikishwa na hii tume ya upigaji kura. Watu wengi waliogopa na wakasema sio tume inaweza kutumika kuonea vyama via kisiasa lakini tumetoa miongozo ambayo itafuatwa. Tumependekeza kwamba chama cha kisiasa ambacho kitaandikishwa kiwe ni chama ambacho kitaweza kukuuza umoja wa nchi yetu na kitaonyesha wazi wazi si chama cha kikabila na kina wanachama katika sehemu zote nchini na kwamba ni chama ambacho kitazingatia demokrasia na utawala uliofaa. Na kwamba ni chama ambacho kitakuwa kinahakikisha kwamba kuna kura mpaka za mashinani za viongozi ambao ni wa vyama hivyo na vyama ambavyo vitakuwa vinazingatia haki za kibinadamu na haki za kijisia na pia vyama vitakavyoweza kukuuza na kuzingatia Katiba hii ya nchi yetu.

Na pia tukapendekeza kwamba, ikiwa kuna vyama ambavyo ni vya kikabila vya kidini visiweze kusajiriwa. Na pia tukasema vyama vya kisiasa vifutiliwe mbali ikiwa vitajihusisha na vitendo ambavyo vinaweza kuleta chuki na vita katika jamii, chama ambacho kinaweka paramilitary militia, ama wana vikundi kama jeshi la mzee na mambo kama hayo viweze kufutiliwa mbali.

Vyama ambavyo havijaweka hesabu zake na vitabu zake vya hesabu sawa sawa na vyama ambavyo vimekosa kupeana vitabu vyake vya hesabu kwa mkaguzi mkuu wa hesabu wa kitaifa pia vifutiliwe mbali, na vyama ambazo ziliandikishwa kwa njia ambayo isiyo halali.

Pia tumeangalia hii pesa tuliseme zipatiwe na serikali na tumependekeza kwamba kila mwaka serikali iweze kuweka kando nukta tatu ya asilimia ya budget. 0.3% of the national budget kila mwaka itengwe kwa kupewe vyama via kisiasa. Na tumependekeza kwamba pesa hizi zipewe vyama vya kisiasa ambavyo vimekuwa zikizingatia mambo ambayo inatakikana vyama vya kisiasa ambavyo vitakuwa vimepata zaidi ya asimilia tano ya kura zote zitakazokuwa zimepigwa nchini, 5% of the total votes casted or the previous general election. Na kwamba pesa hizi zitagawanyishwa mara mbili. Asilimia hamsini ya kwanza itagawanyishiwa vyama vyote kwa usawa. Zitakazobakia vyama vitapewa kulingana na uzito wa vyama hivyo kulingana na kura walizopata kwa kura zilizopita.

Na pesa hizi tumependekeza kwamba zitumiwe na njia ifuatayo:- Kwa kuweza kufanya campaign, na pia asilimia kumi peke yake ya pesa hizo ndiyo zitumike katika kugharamia garama ya kuendesha chama. Na hizo zingine zitumiwe kwa shughuli ambayo itafaa na mtu yeyote asipewe zawadi kutokana na pesa ambazo zimekuwa zimepewa vyama hivyo.

Chapter ya saba tumeangalia Bunge na kwa wakati huu tumependekeza tuwe na nyumba mbili za bunge, tuwe na National Council na National Assembly au Upper House na Lower House. Wazee zamani mlisikia tulikuwa na senate, sio? Sasa tunapendekeza Senate na Bunge hii ya kawaida. Na pia tumetoa juhudi zitakazo zingatiwa na bunge zote mbili, kwanza kabisa tunasema ziwe na watu watakaonyesha umoja wa nchi yetu na kazi kubwa watakayoifanya ni kuweza kutumia mamlaka yetu katika utawala ulio bora kwa sababu tuliwapatia mamlaka ya kufika pale na waweze kuzungumza na sisi mara kwa mara ili watunge sheria zinazofaa na waweze kupitisha misimamo ya utawala uliositahili.

Tumependekeza pia bunge liangalie matumishi yote ya fedha za umma na pia zitunge sheria na kubadilisha hii Katiba kulingana na chapter ya kumi na nane ambayo mtaona vile tumewaaghisia. Tumesema pia Bunge iangalie mikataba ya kitaifa kabla haijaidhinishwa na Rais, na pia iweze kuidhinisha baraza la mawaziri kabla ya kupitishwa. Iangalie na kuidhinisha mambo kadhaa ambayo yatakuwa yanafanywa na Rais, na pia idhinishe atakayekuwa ni waziri mkuu na watu wengine kama majudge na watu wakuu wa serikali. Pia idhinishe hali ya hatari na pia iangalie na kukuuza demokrasia, utawala wa nchi.

Katika article 106 tumeangalia ni akina nani wataenda katika Upper House ama National Council. Tumependekeza kwamba hii Upper House iwe na wajumbe mia moja, sabini ya hawa wajumbe wachaguliwe kutoka Constituencies ambazo tumeangalia kama districts na sio constituencies kama tunazo zitambua kwa kawaida. Tumetambua, district sabini na tumependekeza watu hawa wapigiwe kura kutoka katika kila wilaya. Halafu thelathini ambao wamebaki tumependekeza kwamba kwa sababu mambo yalivyo endelea kwa miaka arobaini ya uhuru, katika hawa watu sabini pengine tutakosa wa mama kwa mambo tofauti ambayo mnaelewa, kwa sababu nyinyi ndiyo hamtupigii kura, sasa tukapendekeza kwamba viti thelathini vitengwe ili

watakaosimama wawe ni akina mama na wasimame tu katika province ama mikoa na sio constituency. Na kila mkoa isipokuwa mkoa wa Nairobi utapewe nafasi nne. Na Nairobi itapewa nafasi mbili.

Halafu katika article ya 107 tunaangalia lower house au National Assembly na tunapendekeza kwamba tuwe na kura za kawaida za constituency tunazozijua ambapo tutapata waakilishi mia mbili na kumi. Lakini tukapendekeza pia, kwa sababu hawa watu 210, wakati mwingine huwa hawajakilisha sehemu zote na jamii zote na watu tofauti kwamba tuwe na watu wengine tisini ambao watapendekezwa na vyama vya kisiasa. Propotional representation ambayo itatolewa na list ya vyama vya kisiasa. Na mambo haya yanafanyika kwa mfano nchi ya South Africa, wana chagua MPs kwa kufanya hivyo, wao hupigia kura vyama. Sasa tunasema vyama vitakaokuwa bunge, vipewe nafasi kulingana na uzito wa vyama kuchagua watu wengine tisini na watu hawa wachaguliwe tukizingatia akina mama, watu walemavu, vijana, makabila na watu walio tengwa. Wakati huu vijana wanasema hawajawakilishwa bungeni watu walemavu wanalia hawajawakilishwa bungeni, akina mama pia wanasema sisi ndiyo wengi lakini tunawakilishwa na mama tisa peke yake njiani. Na tumependekeza kwamba hii list ikitolewa na chama ikiwa chama kimetoa list ya watu kumi waandike list hao kulingana na watu ambao ni muhimu na ni lazima wachaguliwe. Ikiwa list itahitajika watu tano wachaguliwe wa kwanza tano na hii list pia tunapendekeza ikiwa mtu wa kwanza ni mama wa pili awe ni mwanaume hadi kufikia mwisho wa list hiyo. Na watu ambao watakwenda bunge hili la National Assembly, wawe ni Wakenya ambao wana miaka ishirini na moja kuzidi, watakokwenda katika senate au National Council wawe wana miaka thelathini na tano na kuzidi na wawe ni watu wana elimu ya kiwango cha kidato cha nne na wanaweza kuzunguza Kiingereza na Kiswahili sanifu.

Na ikiwa ni watu ambao hawajiwezi, wawe wanaelewa lugha ya ishara, au wanaweza kutumia drill. Na pia viongozi hawa ni lazima watimize mambo ambayo tumeyaweka viongozi ambao tumeweka katika Katiba hii.

Jambo lingine katika article 109, linapendekeza kwamba katika bunge hizo zote mbili, kufikia miaka mitatu baada ya kupata Katiba mpya, ni lazima wamama wawe na 30% representation, kwamba Bunge hiyo, ikiwa na wabunge mia tatu lazima mia wawe ni akina mama.

Halafu tumeangalia 112, jinsi ambavyo wananchi wangeweza kuwarudisha MPs nyumbani ikiwa hawakutekeleza mambo ambayo waliotumwa kufanya. Kwanza kabisa tumesema MP ambaye atakuwa ni mgonjwa na awe hana nguvu na hana akili ya kuweza kufanya kazi hizo kwa sababu amepatikana na maradhi aweze kuondolewa katika mamlaka. MP ambaye anakosa kuwa na tabia ambayo ni sawa na ambaye analeta chuki na vita katika constituency yake arudishwe na pia MP ambaye amekibia na haonekani katika constituency aweze kurudishwa kwa kupitia petition itakayoandikwa na asilimia thelathini ya watu waliojiandikisha kupiga kura katika constitutency. Na hapo mkifanya hiyo petition mnaituma kwa Speaker wa National Assembly na yeye ataomba tume ya kupiga kura kufanya uchunguzi mara moja kupitia siku saba na wamjibu kueleza kama hayo mapendekezo ni ya ukweli. Ikiwa ni ya ukweli Speaker atatangaza kufuta kazi huyo MP na kuweza kuitisha kura katika constituency.

Jambo lingine ambalo ningeghusia ni kwamba tunapendekeza kwamba mishahara ya wabunge iweze kutatuliwa na tume ya kusimamia mishahara ya wafanyi kazi wa serikali. Tumependekeza pia kwamba bunge liwe na calender yake na kwamba bunge itawanshizwa wakati ambapo bunge lenyewe litaweza kukumbali na kwamba bunge isivunjwe bila mambo fulani ambayo tumeyaweka hapa kwamba wabunge wamekubali kuenda kwa likizo juu hiyo ni shuguli yao, na kwamba bunge ambayo ni National Council isivunjwe ila kufikia miaka minne, National Assembly kufikia miaka mitano.

Rais amepewa uwezo wa kuvunja bunge lakini ni lazima atumie sheria hii, sio wakati wowote, wakati ambapo miaka minne imeisha na miaka mitano. Pia Bunge imepewa nafasi ya kuweza kusema kwamba haina amani na Prime Minister. Kwamba hawana imani na waziri mkuu na bunge ingetaka waziri mkuu atolewe.

Halafu tukiangalia serikali kuu, tumependekeza kwamba serikali kuu itakuwa na Rais, itakuwa na Makamu wa Rais, Prime Minister na baraza la Mawaziri. Tumependekeza pia kwamba Ministers wachaguliwe nje ya Bunge pamoja na wasaidizi wao. Tumependekeza pia kwamba mamlaka yote isiwe kwa Rais na mamlaka haya pengine yamepewa waziri mkuu. Natumependekeza kwamba mtu atakayetaka kusimama kuwa na cheo cha Rais awe ni Mkenya na awe amepitisha umri wa miaka thelathini na tano na asipitishe umri wa miaka sabini. Ingawa pia tumependekeza kwamba ikiwa Katiba hii itaundwa na kutumika upigaji wa kura ujao umri huu ya miaka sabini usitumike wakati huu kwa sababu hatukutaka kuambiwa ya kwamba tumetumika kuondoa watu fulani katika utawala. Kwamba mambo haya yafanyike wakati wa kupiga kura ujao.

President atasimama na mwenzake , running mate, huyu President akichaguliwa, yule mwenzake atachukua sehemu ya makamu wa Rais. Na pia tukapendekeza kwamba Rais akisha kuchaguliwa bunge limeanza shuguri zake, Rais ataweza kupendekeza Waziri Mkuu kutoka kwa chama ambacho kina nguvu zaidi katika parliament na kwamba akisha pendekeza hili jina haiwe automatic anarudi kwa Parliament kama Parliament imekubali mtu huyo. Ikiwa Parliament imekataa na kusema kwamba haina imani na mtu ambaye amechaguliwa na Rais, sasa itabidi mkuu wa opposition kupatiwa nafasi ya kuweza kuchagua mtu ambaye ama kupendekeza, mtu ambaye anaweza kuwa ni Waziri Mkuu na hapo bunge ikakagua na kuona kama ina imani na huyo mtu. Ikiwa hawana imani na huyo mtu ataombwa kuchagua mtu yeyote katika bunge kusimama ni kuwa waziri mkuu.
Tumependekeza kwamba Waziri Mkuu awe na naibu wawili na kwamba mawaziri wasizidi kumi na watano na manaibu wa mawazi pia wasizidi kumi na watano.

Na tukiangalia kwa kifupi majukumu ya bunge, niliwaeleza kwamba bunge litakuwa linatakiwa kuidhinisha mambo mengi, for example tumesema kuidhinisha uchaguaji wa waziri mkuu, kuidhinisha uchaguaji wa mawaziri, pia kuteuliwa kwa watu bali bali katika serikali bunge pia itatakiwa kukagua na kuangalia makisio ya fedha za serikali budget, bunge pia linatakiwa kutunga sheria za nchi ambazo sheria hizi zitapatiwa Rais kuidhinisha na Rais amepewa nguvu mara tatu ya kufanya kabla hajaidhinisha sheria ambazo zitakuwa zimepitishwa kwa bunge. Kwanza anaweza kusahihisha mbila kusema chochote, pili anaweza kurundisha sheria hiyo kwa bunge na kutaka mambo fulani yafanywe, tatu anaweza kukataa na kuomba maoni ya mahakama

kuu – Supreme Court.

Bunge pia ni lazima idhinishe hali ya hatari, hari ya vita... **end of tape 1**.

.... jukumu ya Rais na jukumu itakayopewa Prime Minister. Jukumu ambalo ni lazima kwa Rais ni kulinda uhuru wa taifa letu na pia kulinda na kutetea kanuni za sheria. Pia analazimika kuidhinisha sheria, ana majukumu mengine kwa mfano analazimika kuhotubia bunge mara moja kwa mwaka. Rais pia ana haki kama nilivyomwambia ya kuomba mashauri au maoni ya kikatiba kwa korti kuu- Supreme Court. Atakuuza demokrasia na kuhakisha fedha za nchi yetu zina njia inayostahili. Rais pia amepewa majukumu kwa mfano, ni lazima aelezewe mara kwa mara kuhusu utawala wa serikali na Waziri Mkuu ndiyo atakuwa msimamishi wa serikali atakuwa ni amri jeshi wa majeshi ya nchi yetu, msimamishi wa baraza la usalama na taifa, atatangaza hali ya hatari kama itakayodhinishwa na bunge, atatangaza vita baada ya vita kuidhinishwa na bunge, ataweza pia kuwapokea mabalozi na kuteu mabalozi, ataweza kutoa misamaha rasmi pardon of mercy, ataweza kutoa tuzo zinazostahili za kitaifa na ataweza kuongoza kwa kufungwa bunge kulingana na utalatibu tuliotoa.

Naye Waziri Mkuu jukumu lake kubwa ni kuwateua ama kupendekeza majina la baraza la mawaziri na manaibu wao, atakuwa yeye ndiye anatoa na kusimamia kupitia bunge makadilio ya matumishi ya nchi, yeye ndiye atakayekuwa anasimamia shuguli za kiserikali za kawaida, anashuhurutishwa kuhudhuria bunge kwa niaba ya serikali, yeye ndiye atakayeanshisha mswaada ya kiserikali na atakuwa ni mwenyekiti wa baraza la mawaziri. Hiyo ndiyo kazi ya Waziri Mkuu kwa ufupi mtaendelea na kusoma kazi zake ambazo ni nyingi zimewekwa hizi articles.

Pia tumeeleza shuguli za Makamu wa Rais na tumesema kwamba atakuwa ni msaidizi mkuu sio naibu, msaidizi wa serikali, principle assistant of the president. Na pia ikiwa mtu ambaye ameteuliwa kuwa Rais akifariki makamu wake atachukua uongozi wa hiyo ofisi mara moja kabla hajateuliwa Rais mwingine. Na pia tumeeleza jinsi ambavyo Rais anaweza kuondolewa mamlakani na tumesema kwamba ikiwa Rais amekosa atatolewa wakati ambapo 2/3s of parliament itapitisha motion ya kusema hafai na anafaa kushtakiwa katika Supreme Court na hapo kupitia kwa Speaker, Speaker atakagua na kuita National Council ambaye itakagua mashtaka haya na ikiwa National Council itakubaliana na kupitia kura two-thirds, Speaker atapendekeza mambo haya kwa mkuu wa sheria ambaye ataweza sasa kuwanshisha kesi rasmi bidi ya Rais ili aweze kuondolewa mamlakani. Prime Minister naye kutakuwa na hiyo vote of no confidence, kwamba bunge halina na imani na yeye au pia anaweza kujiuzulu ikiwa hataki kuendelea na kazi hiyo.

Katika chapter ya tisa tumeangalia mahakama na tumependekeza kwamba tuwe na korti ingine juu ya korti ya appeal ambayo tumeita Supreme Court na tumependekeza misimamo itakayopendekezwa na wafanyi kazi wote ambao ni wafanyi kazi wa korti. Tumependekeza kwamba Supreme Court iwe na Judge ambao sio zaidi wa sita. Tumependekeza kwamba Court of Appeal kuwe na Judge wasio zidi kumi na wakiketi wawe ni Judge watatu ambao wanaketi katika court of appeal.

Tumependekeza pia qualifications za watu ambao wanaweza kuchaguliwa mukiangalia article 195 na tukapendekeza kwamba

Judge waweza kufanya kazi yao na kushtaafu wakiwa na miaka sitini na tano. Lakini Judge akifika miaka sitini apewe ruhusa wa kushtaafu ikiwa atapenda mwenyewe. Tumependekeza kwamba pia judge aweze kuondolewa ofisi ikiwa ameshidwa kwa ugonjwa kufanya kazi zake ikiwa ana tabia isiyo faa, ikiwa inaonekana amekosa kuwa muadhirifu kwa kazi yake na tumependekeza kuwa tuwe na tume itakayosimamia hiyo juhudi ya hiyo mahakama ambayo ni Judicial Service Commission tunayo wakati huu lakini tumeipatia nguvu zaidi na tumependekeza kwamba hii Judicial Service Commission ndiyo iwe na uwezo wa kupendekeza watu watakaoteuliwa kuwa majudge na kwamba mara kwa mara waangaliwe tabia za watu wanofanya kazi kwa mahakama na pia ikiwa kuna mtu yeyote amekosewa ataweza kushtaki hii Judicial Service Commission ambayo itamuomba Rais aninshishe kesi ambayo itachungulizwa kumuondoa judge katika ofisi yake.

Tumeangalia pia ofisi ya Mkuu wa Sheria na kupendekeza kwamba ofisi hii iweze kugawanyishwa mara mbili. Tumependekeza kuwe na ofisi ya mkuu wa sheria ambaye kazi yake hasa itakuwa ni kutumikia serikali na kuweza ku-advice serikali kuhusu mambo ya serikali na taifa na ofisi nyingine ya msimamishi wa kesi za umma, Director of Public Prosecution iwanzishwe. Kwa sababu ikiwa mtu ndiye advisor wa serikali tena ndiye anaambiwa wakati mwingine kusimamia kesi pengine wa upinzani wa serikali, tunaona hapo wakati mwingine hapo hakuna haki inayotendeka ama ikitendeka hatuioni kwa sababu wa msongamano wa kazi na tukasema kwamba huyu Director of Public Prosecution ndiye asimamie kesi zote za umma.

Pia tukapendekeza msimamishi wa haki za wananchi, public defender ama Ombudsman na tukasema kwamba kuteuliwe mtu na Rais kwa kupitia Judicial Service Commission atakayekuwa ni msimamishi wa haki za wananchi na ataweza kuwapatia advice wananchi na kuwapatia representation wakati mwananchi hawezi kuweka wakili, na pia mwananchi akikosewa atakuwa na ofisi ya kuenda na kulalamika. Tukaangalia pia shuguli za mawakili na tukapendekeza pia shuguli hizi ziwekwe kwa katiba kwa sababu hawa ni watu ambao wanastahili kuhifadhi na kutetea haki za wananchi na tukapendekeza kwamba haki yao muhimu ni kutetea na kusimamia Katiba ya nchi. Pili ni lazima waheshimu na kukuuza haki za kimsingi, tatu wasimamie kazi yao kwa uwaminifu na uwabijikaji kwa wananchi na pia wakiwa katika kazi yao waifanye na kutetea wateja wao bila uoga, na pia ikiwa kuna maneno ama karatasi yeyote muhimu ambayo haitamudhuru mtenja wake ni lazima wakili aitoe kwa korti na kusaidia korti iweze kutoa hukumu ambayo ni ya haki. Sasa hiyo ndiyo kazi ya mawakili waliopewa na katiba.

Tukiangalia chapter ya kumi tutaangalia utawala mashinani. Devolution of power na katika article 213 tumejaribu kueleza kazi ama misimamo itakayozingatiwa na hizi serikali za mashinani. Tumependekeza kwamba hizi serikali zinafaa kuleta utawala karibu na wananchi na kuwapatia wananchi nafasi ya kujihushisha na utawala wa nchi.

Tumependekeza kwamba pia zijaribu kukuuza nafasi yetu kama wananchi katika utawala na pia zijaribu sana kuzingatia demokrasia na kuweza kuhakikisha kwamba kuna maendeleo ya kiuchumi na kijamii, zihakikishe kwamba rasilimali na pia mali zote za nchi zimegawanyishwa kwa usawa lakini pia serikali iweze kukuuza sehemu ambazo zimetengwa, na pia zijaribu kuhakikisha kwamba huduma zinawafikia wananchi kwa njia inayoshtahili, na kwa njia ambayo sio gharama ya juu na pia kujaribu ku-protect, na kuchunga masilahi ya watu ambao wametengwa, disadvantaged na minorities katika sehemu mbali mbali

za nchi.  Na tukapendekeza kwamba  tuwe na serikali aina nne.

Tumependekeza kwamba kuwe na serikali ya vijiji ambako kutakuwa na wazee sita wa vijiji ambao watatawala katika kijiji na ikiwa kuna kijiji ambacho pengine hakina imani na wazee wa kijiji hicho wachague watu wasio zidi kumi na wasiopungua sita kuweza kutawala kijiji.  Na kwamba watu hawa waweze kuangalia jinsi watakavyopendelea kutawala vijiji hivyo kuzingatia mambo ambayo tumesema au misimamo ambayo ni ya utawala.  Halafu tumesema ya kwamba tuwe pia na serikali ya kata au locational government, na kwamba katika kila location serikali hii iundwe na representatives wawili  kutoka katika kila kijiji.  Na kwamba hawa representatives ni lazima mmoja awe ni mama. Lakini kijiji kikitaka kutuma wamama wawili sheria haijakataa lakini hamuwezi kutuma wazee wawili lazima mmoja awe ni mama. Halafu pia tumependekeza si nyumba pia ina wazee na wamama sasa tunasema pia serikali ni hivyo.

Tunapendekeza pia kuwe na msimamishi wa shuguli za kata ambaye ataweza kuchaguliwa, halafu tunapendekeza tuwe na serikali ambayo ni ya wiraya itakayo simamia location na vijiji na watu ambao watakuwa ni watawala katika district tunapendekeza wachaguliwe kwa kupitia kura na watu hawa wawe ni thelathini au ikizidi izizidi ishirini na wawe na msimamishi administrator ambaye atachaguliwa pia kwa kupitia kura.  Pia tunapendekeza kuwa uwezo mkubwa wa utawala uweze kuwa katika district.  Na kwamba district isimamie kuchukua fedha na mambo yote ambayo  ya stahili kufanyika katika hiyo location.  Kwa mfano hospitali, mabarabara, mashule, masoko  na mambo kama haya yote yasimamiwe na district.

Pia tumependekeza tuwe na serikali ya mikoa lakini serikali hii haitakuwa na nguvu zaidi ya serikali ya district na kazi yake tumependekeza iwe nikusaidia wilaya katika utawala, kuwapatia elimu na ushauri utakaoweshesha serikali za wilaya kutawala kwa njia iliyo nzuri nakuwasaidia pia kutengeza plan ambazo zitawaweshesha kutumia rasilimali ya mkoa huo kwa njia iliyofaa.  Na pia ikiwa mkoa una mashirika tofauti basi serikali ya mkoa itaweza kutumia nafasi hiyo kuangalia  mashirika hiyo tofauti.  Na ukiangalia katika schedule huku nyuma tumeeleza katika schedule ya saba jinsi kutakuwa na utawala wa National Government na pia District Government kwa sababu tumesema district government ndiyo itakuwa na nguvu zaidi kwa hivyo tumeeleza jinsi serikali hizo mbili national na district zitakuwa zinatawala.

Chapter ya kumi na moja tumeangalia mambo  ya mali na mashamba, tumependekeza kwamba mara kwa mara serikali iwe inaangalia jinsi ambavyo mali na mashamba inagawanyishwa  na jinsi ambavyo tunatunza na kutumia mashamba yetu na jinsi ambavyo tunachunga mazingara na mashamba hayo.  Tumependekeza kwamba kila Mkenya awe na haki ya kuweza kumiliki mali na kwamba mtu ambaye siye Mkenya asiweze kuwa  anamiliki mali lakini aweze kukodi shamba kwa miaka isio zidi tisaini.  Na pia tukaweze kupanga aina tofauti za sheria  au umiliki wa mashamba.  Tumetambua kwamba kuna mashamba ambazo ziko chini ya serikali ambazo ziko katika kifungu cha sheria mia tatu na moja, the government's land act, tumetambua kwamba kuna mashamba ambayo yanasimamiwa na mashirika bali bali za kiserikali.  Tumetambua kwamba kuna mashamba ambayo yanasemekana kama ni trust land, ambayo yanafaa kusimamiwa na jamii tofauti, na pia tukapendekeza kwamba mashamba ambayo ni ya umma yawe yanasimamiwa na tume ya mashamba ili kuyahifadhi na kuhakisha mashamba hayo ni ya manufaa

kwa wakenya yote kwa wakati huu na siku za usoni.

Na tumependekeza kwamba serikali ihakikishe kwamba kuna sheria ambazo zitaweza kutunzwa mashamba na mali ambayo ni ya watu tofauti. Na katika kupendekeza kuwe na Tume ya kusimamia mashamba tumependekeza kwamba Tume hii iwe na kati zifuatazo. Iwe ndiyo inasimamia mali yote ya umma, iwe ndiyo inahakikisha matumishi ya mashamba ya umma, iwe inaangalia mara kwa mara misimamo ya kitaifa, uza mashamba, ijaribu kuangalia sheria kwa sababu tuna sheria nyingi za mashamba ili kuhakikisha kwamba sheria hizi zina ambatana kwa sababu kwa wakati huu hazizikizani na hizo, na pia tunapendekeza waweze kuangalia mizozo iliyoko kuhusu shamba. Kwa mfano kuna mzozo tofauti tunaisikia hasa kwa upande wa sehemu hii yenu, upande wa Pwani, upande wa Rift Valley na North Eastern. Kuna mizozo mingi ya mashamba na tumependekeza tume hii iangalie mizozo hiyo ili serikali iweze kutatua mambo hayo.

Na pia tumeangalia tafsiri ya shamba. Shamba ni kitu gani? Mtasoma na kuangalia tafsiri hiyo ka sababu kwa wakati huu kuna watu ambao wanasema mimi hii nyumba ni yangu lakini shamba sio yangu, upande wa Mombasa, una nyumba lakini mwenye shamba ako sehemu za Uarabuni. Sasa tunaangalia je shamba ni kitu gani? Ni ardhi peke yake ama ni vitu vyenye chini ya ardhi au juu ya ardhi kama kwenye anga ambayo inapita kwenye ardhi yako na tumeeleza kwa kifupi katika article 238.

Katika chapter ya kumi na mbili tumeangalia mazingara na mali ya asili na jinsi ambavyo serikali itakuwa na jukumu ya kuchunga vitu hivi pamoja na sisi kama wananchi.

Katika chapter ya kumi na tatu tumeangalia fedha za umma na tumependekeza kwamba bunge isimamie fedha zote za umma na matumishi yake. Tumependekeza pia kwamba deni zote za serikali zikaguliwe na bunge kabla serikali haijachukua madeni hayo. Pia tumependekeza kwamba kuwe na sheria ambazo zita simamia Benki kuu na shuguri ya benki kuu na mtu atakayeteguliwa kuwa ni governor wa Benki kuu. Pia tumependekeza kwamba mkaguzi na msimamishi wa fedha za umma ofisi yake igawanyishwe mara mbili. Tumesema kwamba ofisi hiyo igawanyishwe na msimamishi wa makadirio na matumishi ya fedha ya umma, controller of budgets, na mwenzake awe ni Auditor General au mkaguzi wa mali ya umma. Moja atahakikisha kwamba pesa zimetumiwa kwa njia iliyopitishwa na bunge na mwingine atakagua kuhakikisha kwamba fedha hizo zilitumika kwa njia iliyofaa.

Pia tumependekeza katika chapter ya kumi na nne huduma za umma jinsi ambavyo wafanyi kazi wa serikali wanafaa kuhudumu kwa wananchi. Tumependekeza kwamba wawe na misimamo ifuatayo: wawe ni watu watafanya kazi yao na nidhamu ya hali ya juu, wataweza pia kufanya kazi yao kwa njia ambayo haitatuwekea hasara na watakosa kupendelea pia watafanya kazi yao kwa haraka na mara moja watafanya kazi yao kwa uwazi na watawajibikia wananchi na kwamba wakiandikwa waandikwe kwa sababu wamestahili na sio kwa sababu wamejulikana au kwa mapendeleo ya kikabila ama mambo kama hayo. Na kwamba kusiwe na ubaguzi wakati ambapo kunakuwa na training kwa sababu ya kabila lao ama ni wanawake ama ni wanaume wapewe nafasi ya kujiendelesha katika kazi zao na kwamba watu watakaofanya kazi katika sector hii ya umma wawe ni watu

kutoka sehemu zote za nchi yetu mbila kuzindi kabila hili ama lile. Na katika level zote ama ngazi zote za kazi za umma.

Pia tumependekeza tume ya kusimamia wafanyi kazi wa umma Public Service Commission na tukawapatia kazi zao, mtaweza kusoma na kuangalia. Pia katika huduma hii tumeangalia Kenya Police ama ma polisi na tukaangalia msimamo utakaozingatiwa na polisi na tumependekeza kwamba kazi zao hasa ni kazi zifuatazo. Kuweza kuweka amani na kuchunga mazingara, kuweza kuchunga haki za kibinadamu kuweza kuchunga security ya wananchi, kuweza kupunguza na kukagua hali ya uhalifu, na kuweza kuwasaidia watu ambao wamepatikana na madhara, na pia kuchunga mali ya wananchi.

Tumependekeza pia watu wanaohudumu katika polisi wawe ni watu wanaofanya kazi yao kwa nidhamu ya hali ya juu, watu ambao wataepuka na corruption au hongo na rushwa, watu ambao watakua hawambagui na hawatangamani na siasa za upande wote, watu ambao wataweza kuzingatia haki za kibinadamu na wataweza kupewa mafunzo ambayo ni ya hali ya juu kuwaweshesha wafanye kazi zao.

Pia tumeangalia huduma zingine za usalama pamoja na wanajeshi tofauti. Tumeangalia polisi wa utawala, jeshi la ulinzi, jeshi la wanamaji, jeshi la wanahewa na kikosi cha upelelezi. Na tukasema hawa pia watafuata msimamo ambao tuliweka kwa kazi za watu ambao wanahudumu katika polisi.

Jambo lingine ni kwamba tumependekeza jina la magereza kubadilishwa kutoka kwa Kenya Prisons ili iwe inajulikana Kenya Collectional services. Na tukasema hivyo kwa sababu tumependekeza kwamba kazi kubwa ya magereza ni kujaribu kuwabadilisha wafungwa mbali na kuwaadhibu kuwasaidia ili wakitoka waweze kujiunga na jamii na kuweza kuwa ni wananchi wanamanufaa katika jamii.

Pia tumependekeza katika chapter ya kumi na tano kwamba tuwe na Defence and National Security, tume ya usalama itakayoweza kuzingatia mambo tofauti ya usalama wa nchi, kwa mfano hali ya hatari, hali ya vita.

Katika chapter ya kumi na sita tumeangalia leadership and intergrity kwa watu ambao watakuwa wanahudumu kuhusika uongozi. Tumeangalia ambayo yanawafaa na kuyapasa viongozi kufanya.

Chapter ya kumi na saba tumeangalia vyombo ambavyo tunaviita vyombo via kikatiba - Constitutional Commission na pia Tume ambazo ni za kikatifa na ofisi ambazo ni za kikatiba. Tumependekeza kama mlivyosikia tume ya huduma ya umma Public Service Commission, Tume ya huduma ya mahakama, Judicial Service Commission, huduma ya bunge, Parliamentary Commission, tumependekeza tuwe na Parliamentary Commission na pia tumependekeza tuwe na Tume ya haki za binadamu na haki za kitawala, kwa Kiingereza Human Rights and Administrative Justice Commission, tumependekeza pia tuwe na Tume ya Uchaguzi, Electoral Commission, Tume ya Mishahara na malipo, Salaries and Remuneration Commission, tumependekeza pia tume ya Upangaji wa Hazina, Tume ya Katiba, Mkuu wa Sheria tunasema pia ni ofisi ya kikatiba, mahakama pia

tunapendekeza iwe ni ofisi ya kikatiba, mkurugenzi wa mshitaka, Director of Public Prosecution, mtetezi wa umma, Public Defender, Governor wa Benki Kuu, msimamishi wa makadilio na mapato, Controller of Budget, mhasibu mkuu wa hesabu za kitaifa, Auditor General, na pia Tume ya Ardhi. Kwa hivyo tumependekeza Tume kama mnavyoona ambvyo ni tume nyingi za kikatiba ambazo zitasaidia serikali katika shughuli zake za kuweza kuwa na utawala bora.

Pia tumependekeza katika chapter ya kumi na tatu jinsi ambavyo tutaweza kubadilisha katiba itakayopitishwa na tumependekeza kwamba bunge iweze kubadilisha katiba hii kupitia two-thirds majority ya members wa parliament, lakini tukasema kwamba hawa wasiwe na uwezo wa kubadilisha katiba mzima. Na tumependekeza kwamba articles zifuatazo sisibadilishwe na bunge, bali ziletwe kwa wananchi kwa kupitia kura ya maoni.

Tumependekeza kwamba article ya saba inayozungumza kuhusu mipaka ya nchi yetu, pia tumependekeza article ya kwanza inayozungumzia mamlaka ya wananchi, tumependekeza pia chapter ya sita, ambayo tumezungumzia maadili na misimamo ya kitaifa, tumesema pia chapter ya tano inasimamia haki za kimsingi, na pia tumesema kifungu ambacho kimesimamia uwananchi au citizenship usiweze kubadilisha na bunge na pia hii chapter ya kumi na nane isiweze kubadilishwa na bunge bali mambo hayo yaletwe ili wananchi waweze kuangalia na kupitisha.

Katika chapter ya kumi na tisa tunaangalia maneno ambayo tumetumia na maana yake, pia tumeangalia katika chapter ishirini, transitional and consequential provision, au mambo ambayo yanafaa kuwezesha kutoka katiba hii, na kuingia katiba nyingine. Baada ya hapo tumekuwa na schedule ya kwanza tunaangalia mipaka tofauti ya nchi yetu.

Schedule ya pili tumeangalia mikoa na wilaya tofauti ya nchi yetu. Schedule ya tatu tunaangalia national symbols ua vifaa vya kitaifa, schedule ya nne tumeangalia na kupendekeza viapo vitakavyochukuliwa na viongozi tofauti.

Halafu katika schedule ya tano tumeangalia misimamo na mambo ambayo tunatakiwa kuzingatiwa na viongozi. Leadership and Intergrity code ambayo ni mitihani ambao viongozi wote ni lazima waupite.

Halafu katika schedule ya sita tumeangalia mambo ambayo ni lazima yatumikiwe na bunge, ili kuweshesha hii katiba yetu ikamilike na kutumika kwa njia iliyostahi. Kwa mfano tumeangalia mambo ya mashamba na tukapendekeza kwamba bunge itatue mambo ya mashamba kwa kufikia miaka miwili.

Schedule ya saba tukaangalia mamlaka ya serikali kuu na serikali za wilaya. Katika schedule ya nane tumeangalia mambo yote ambaye tunadhania ni muhimu kuweza kuondoka katika utawala wa Katiba mzee kuingia katika Katiba mpya. Kwa mfano tunaangalia mambo yanayohusu sheria za wakati huu, tunaangalia haki na majukumu ya kiserikali, tunaangalia upigaji wa kura, tunaangalia vyama via kisiasa kwa sababu tunaangalia vingi hazijazingatia mambo ambayo tumependekeza na tumewapatia miezi kumi na miwili kuweza kuzingatia sheria za kikatiba. Tunaangalia devolution of power, tunaangalia serikali kuu, tunaangalia

administration kwa sababu mataona kwa wakati huu hatukupendekeza provincial administration, je watu hawa chief kufikia PC watakwenda wapi na wako kila sehemu za nchi yetu na tukapendekeza kwamba watu hawa warudishwe kuwa ni wafanyi kazi wa umma. Wawe re-deployed kwenye public service. Tumeangalia pia watakaotaka kustaafu kwa sababu ukimwambia PC lazima uende kwa Office of the President ataona hayo ni mambo magumu. Je watu kama hawa walipwe kivipi.

Tumeangalia judiciary, tumeangalia pia wafungwa ambao wamehukumiwa kifo je watafanyiwa nini kwa wakati huu. Tumeangalia pia kuundwa kwa vyombo hivyo via kikatiba. Sasa kwa kifupi sana ni hivyo au mambo hayo mambo ambayo tuko nayo katika mapendekezo ya katiba mpya ya nchi yetu. Na pengine vile ningesema kwa vile nimeongea saa nyingi niwapatie nafasi watu ambao ningetaka nifafanue mambo ambayo hamkuelewa kwa sababu nina hakika wengi wenu mlikuwa mmesoma hii katiba na pengine mambo ambayo mngetaka tufafanue zaidi ama kama kuna maswali ama kama kuna mjadala au pengine ni mhimu kwa kujitayarisha, kwa kuwatuma delegates wenu katika National Conference.

Na ikiwa kuna watu wangependa kuzungumza tunawaomba waje hapa mbele kuna kiti pale na watuambie majina yao na kuweza kuzungumza kupitia kwa microphone kwa sababu tuna nasa sauti ili tuweze kutoa report ya mkutano huu wa leo, na ukimaliza kuzungumza utakwenda pale kwa Bw. Mukewa kujiandikisha ili tuweze kupata majina yenu kwa njia iliyo kamilifu. Sijui kama kuna watu ambao ama pengine mmetosheka tufunge mukutano. Mmetosheka? Mzee pale.

**Jonathan Muia:** Nashukurua sana kwa nafasi hii nimepewa kwanza ile ningetaka nizungumzie ni elimu. Kwa jina ni Jonathan Muia wa Muoki. Jambo lile ningetaka kushikiria na liangaliwe ni elimu ya watoto. Tumesema kutoka primary mpaka upper education lakini unaona nchi zinaendelea na technology hiyo mambo ya ufundi haikuwekwa mkazo kwa sababu tuna ufunguvu wa waalimu wa kiiufundi. Shule nyingi zile ziko especially Makueni hakuna waalimu wengi wa serikali na pia watoto wangetaka huo mswaada.

Ya pili ni mambo ya kilimo. Tunanjua kabisa utu wa mgongo wa Kenya ni kilimo na hii mambo ya elimu ya kilimo ni kama haikuangaliwa kabisa kwa mashinani. Kunaweza kuwa kwa village hakuna mtaalamu wa ukulima, agriculture, vetinary and any other. Mimi ningetaka hiyo iangaliwe halafu hayo mafunzo yaletwe kutoka provincial mpaka kwa mashinani. Ni hayo tu nasema ni asante.

**David Kimuli:** Natoa shukurani kwa kupewa nafasi hii ya kuzungumza. Mimi nitaanza kuzungumza kuhusu mizozo ya mashamba. Mimi naitwa David Kimuli. Wakati wa ukoloni wazungu walitangaza ya kwamba kama wanataka mtu awe na shamba lake waweke mipaka na wakaweka mipaka mwaka wa 1938 kila mtu akawa na shamba yake. Na tukakaa mbila mizozo yote kufikia mwaka wa sabini na nne wakati survey ilikuja area hii na shida iliyo ingilia wakati wa mashamba yetu sasa hao walivunja ile mpaka ya zamani wakaanza kuweka ingine na iwakafanya watu wengi wafanye makesi na mpaka ya zamani ikaangaliwa na mizozo ya mashamba ikaanza. Sasa maoni yangu ni kwamba kama inawezekana ile mizozo ya zamani irudishwe ninaonelea ya kwamba mizozo huenda ikamalizika. Naye kutokea 1938 mpaka 1974 kila mtu alikuwa na shamba

yake na akaweka development mpaka kila kitu mzozo uliokuja juzi mwaka wa 1974 sasa ikawa ni shida mtu kuwa na shamba yake na ameka development amepanda miti, amefanya hii, na ikawa ni shida. Kwa hivyo maoni yangu ni kama makesi ya shamba itaendelea irudiwe ile mipaka ya 1938. Asante.

**John Mulwa:** Asante sana Commissioner. Yangu huenda ikawa ni maswali tu. (interjection)

**Com. Abida**: Jina lako?

**John Mulwa:** Naitwa John Mulwa, ningelipenda kuuliza swali kama hili hapa ulipokuwa ukiongea sijasikia ukiongea habari ya utangazaji, Ministry of Information. Habari ya utangazaji hapa nchi Kenya sijui kama iko ndani ya katiba ama namna gani. Tunapotangaziwa habari hapa nchi tunasikia habari za watu wachache sana ama watu kadhaa ambao sijui ndiyo utangazaji unapendelea ama ni vipi na tunahitaji kusikia habari za kila upande kwa kila mtu. Hata pengine hawa wanaoendesha kazi hii ya katiba tungependa kusikia kila mara mnaendelea aje habari hatusikii.

Swali lingine ningelitaka kuuliza ulitwambia ya kwamba mtatuletea magazette ambayo mlichapisha yalioandikwa kwa lugha ya Kiswahili utatuletea lini na kwa njia gani kwa maana sisi hatutoki hapa kutoka mahali mbali mbali na kuna watu ambao wanategemea sisi wanjue habari ya Katiba vile ilivyo. Kwa hivyo mtuhakikishie ama mtuulize mtatuma mahali gani.

Swali lingine ambalo sijasikia ukiongea mambo yake ni ya usafiri. Hapa nchi Kenya kuna usafiri wa aina nyingi, kuna usafiri wa ngari moshi, mabasi, matatu, magari ya watu binafsi na hapa ikiwa. Kwa bahati mpya, mtu au jamaa fulani amepata ajali ukienda kufuatilia watu wake unaambiwa hiyo ngari haikuwa na insurance. Kama ni ngari moshi, hatujui kama ina insurance ama ni vipi sasa hapa tungelipenda kujua mwananchi wa Kenya atalipwa vipi ili ikiwa ametoka kwa ngari gani ama ajari fulani lazima walipwe. Hiyo ni swali moja ambalo ningetaka kujua.

Jambo lingine nilikuwa nimetayarisha lakini nimeona kama umeongea baada ya kueleza ni uchaguzi. Sasa uchaguzi tunachagua watu lakini tuna uchaguzi mbali mbali kwani ikiwa hapa tunaambiwa tuchague mtu fulani awe kiongozi wetu tunaambiwa wale wanataka fulani tunainua mikono sasa huyo sio pengine uchaguzi wa maoni ya mtu. Uchaguzi wa aina hii haufanywi. Kwa hivyo uchaguzi kuwe na uhuru wa kuchagua si kulazimishwa ama kuambiwa. Uhuru wako mwenyewe unaona fulani ndiye anafaa uchague ule ule tu na uchaguzi wowote utakaofuata baada ya uchaguzi hii kuanza uchaguzi wowote hapa nchini Kenya uwe huru na wa siri sio kuchagua ukiambiwa, ama tuambiwe mtu ni huyu tunataka huyu hapana uliza tutachagua wa siri.

Lili lingine ni vyama vya kisiasa. Nimeongea mambo ya vyama vya kisiasa kwa vile nilikuwa nafikiri maoni ya wananchi. Nimeona hapa nchi Kenya vyama vya kisiasa vilikuwa vingi ambavyo hazifai. Vyama arobaini na nane na hata zinaendelea kupanda hii inaonyesha kila district iko na chama chake ama kila kabila kwa maana makabira hapa Kenya ni arobaini na mbili ama arobaini na tatu sasa kila kabira itakuwa na chama kimoja hata viwili sasa hizi vyama vyote vitakuwa vikifanya kazi gani?

Tungelipenda hata wale wengine wanaona kama mimi vyama viwe vitatu vikizidi viwe nne nchi iwe tulifu maana hivi vyama vyote ni zakutenganisha wananchi. Nafikiri wenzangu wanaweza kuniunga mkono.

Kuna jambo lingine ufisadi- hongo.... **end of side 2A** .... hatujafahanishwa kikatiba vizuri sana. Ukienda pengine sijui matatuambia aje, court unapenda kortini unaenda kushtaki kesi yako na hapo unaambiwa kesi yako kuandikisha ni pesa kadhaa halafu unatoa pesa. Ukitoa pesa karani anakwambia kuna jambo lingine fulani hapo, hujatimiza leta pesa kadhaa unampa, kumbe hizo si pesa zinajulikana kwa serikali. Ni karani tu haya anakwambia kesi yako ni kipeleka korti inataka pesa kadhaa unajua ulete na hujui ni nini kinaendelea hapo wewe unanyanyaswa tu. Hongo inaendelea hata ndani ya korti sasa katiba mtahakikishasa kwamba mambo haya yatakoma kama kortini kutakuwa na hongo je mwananchi atakua vipi? Kwa hivyo ikiwa mnaweza kwenda kujadiliana hiyo la korti pengine judicial court ama judicial commission iwe ikichapisha malipo ya korti ni haya, mwananchi akifika aone malipo ya korti ni haya. Kwa hivyo akiwa ategemea wale makarani, hao ndiyo wamezidi kabisa. Nilikuwa na hayo maswali tu.

**Justus Levi:** Majina ni Justus Levi. Nilikuwa nataka unifafanulie government, what will be the composition of our government? Kwa sababu nimesikia tumekuwa na mention ya very many governments from village to the national level so what will be the composition of the government? Kwa nini niulize hii swali ni kwamba as far as mimi naelewa the government should have its composition perhaps ministers and all that and Kenya we have been having local government term being given as local government which is really not a government. Local government are not governments. The term though tulichukua kwa kikoloni na tukaileta kwetu.

Na kile kingine 171, there is a Prime Minister, we have seen how the Prime Minister will be appointed how about the ministers, how will the Ministers be appointed? Tutawachia Rais, tutawachia, Vice President, Tutawachia Prime Minister it is not clear here. Then there is 162, there is the protection of the President. The President is heavily protected here and in case of President committing crimes it is not clear. I am proposing instead of jus cabinet or whoever, we should have a public referendum kwa sababu amechaguliwa na wananchi let the public participate in removing him.

In Judiciary 184, a lot has been touched but the arm that should protect wananchi the public there isn't. Inaonekana ni lazima uende kwa korti na korti ni lazima uwe na connections usipokuwa na connections ama hiring of lawyers (interjection: inaudible) I am saying we should have a consumer court at locational or divisional level and a consumer court should be headed by a retired reputable Judge. He should be accessible to the public tukiwa iko kwa location kama hapa kwetu kwa chief tuwe tunaweza kumuona every time. Kwa sababu mwananchi akikosewa hapa bara barani korti kwetu ni mbali sana.

In 176, I was feeling that attendance of Parliament by Ministers should also be regulated. The minister should attend parliament required number of attendancies because even today we have got a lot of ministers who do not attend parliament even when there are questions they should be answering and when a minister does not attend parliament it should be clearly stipulated what

disciplinary action should be initiated and the public should be involved.

In the boundaries of Kenya and the laws related to border, Lake Victoria Kenya has a small part which is not... it should be bigger than that and the waters of Lake Victoria, Egypt and the North African Countries have a say. This thing has not become clear to the public and even we hear that the water flowing into the rivers that are flowing into Lake Victoria to North Africa they have some say.

The other is land ownership. We have had state land that was orginally owned by the government and has been captured by some individuals. I am recommending recovery of that land. Because I am sure wale ambao wamechukua they must have spoiled dates. They must have destroyed the title deeds or there is a lot of government land that has gone and properties also.

I feel that the Administrative Police and Kenya Police should be merged because the roles are not very clear. Why have two forces? For the commissions I feel we should increase medical commission kwa sababu if we do not have good medical services the national health burden will be very heavy and it will deteriorate into the national reserve.

Citizenship I feel that citizenship by registration which has been issued within the last 20 years should be reviewed especially Wahindi, Wasomali kuna wengi ambao wameingia nchini kwa njia za ukora.

There is another aspect I am proposing of trade standards. We should have protection of Kenyans against the non-Kenyans on trade especially patterns. A lot of Kenyan products are have been patterned abroad. Kama chondo has been parttened by somebody in Japan and if any Kenyan want to sell chondo, in USA, he has to have permission from Japan today, while it is our indeginous product.

The other thing is protection of indeginous knowledge, properties, medicine and culture. That has not be in touch with the constitution.

Finally, I have not heard mention of provision of facilities such as electricity, telephone by the state because these are very important, energy, is one of the factor that contribute to sustainable development. Bila energy we cannot have development and in the coming technologies the constitution has not mentioned anything about information technology. Information technology is the one that is taking over the world and if Kenyans are not going to be protected or we are not going to have guidelines in information technology then we will be left in an island probably where we cannot move fast. Thankyou.

**Martin Kisenga:** My name is Martin Kisenga na nataka kuzungumzia mambo kidogo juu ya kwanza vyama via kisiasa. Vyama vya kisiasa havikuwekwa limit kama vitakuwa ni ngapi na tukisema vyama vitakuwa vikipewa pesa ya serikali hata mimi na mwenzangu tukitoka hapa tunaweza kuunda chama chetu na tu-register na tupewe pesa. Kwa hivyo hapo ingepaswa

muangalie na mfafanue ni vyama vingapi ndiyo viweze kugawanyiwa zile funds na wasinje wakatumia pesa za serikali kwa njia iliyo mbaya.

Upande ule mwingine ni kuhusu mambo ya administration. Ile nimeona katika hii draft hii nimeona kitu ambacho kitakuwa kina confuse wananchi kwa sababu nimeona kuna serikali ya vijiji, ya malocation, yaani kitu ambacho hakikueleweka vizuri kwa upande wangu mimi. Na mimi nafikiria pia wengine inawatatanyisha. Huyu mtu wataenda kukaa kijijini wachague ambaye watakuwa si binded by law na hawana fine wanaweza kumisuse hizo fedha wako nazo. Kwa hivyo pangalikuwa tu kuna mtu anafanya kazi na anaogopa akiwa anafanya kazi anajua, anaweza kupatikana na hatia, aweza akafutwa kazi au kufungwa. Lakini mtu akiachawa hivyo awe mtu wa kuchaguliwa atakuwa hana hayo.

Tukienda sana kufika kwa council na hapo natatanisha kwa sababu kuna councillors na kuna hawa watu wengine sijui watakuwa ni part of the councillors ama ni watu wengine watachaguliwa wawe wakiendesha mambo yao ya hapo na naona kama watu watakuwa ni wengi kama tutakuwa na councillors na watu wengine tutakuwa tunawachagua mauchaguzi itakuwa ni mengi sana na hatutajua ni wapi tunachagua huyu kwa hii na ile.

Pale pengine ni Parliament, hii parliament sijui ni mimi sikuelewa naona kama kutakuwa na parliament mbili na watu ni wengi sana na hapo naona kuna kasoro kidogo. Mimi ningependelea ile system iko tu.

Kwa upande mwingine ni juu ya holidays. Hii holidays ni sawa lakini kuna jambo ambalo limewekwa hapo maanake nchi yetu kuna kitu si hutaka – heroes day – kitu kama hicho kwa sababu hii nchi yetu ni moja wapo wa zile zilipiganiwa kwa hivyo inapaswa kua na historia kitu ya kuonyesha kweli watu walipigana, uhuru haukupatikana kwa kupitia siasa na kusomeshana ni watu walikwenda msituni na wakapigana na wakamwaga ndamu na ndiyo hii uhuru wetu uakapatikana. Kwa hivyo hatuna chochote cha kuonyesha, na kisasi kilichoko kwa sasa kikiondoka maanake wengi wao waliona na walisikia, wajae hawatakuwa wakijua ni kitu gani kinaendelea kwa sababu hata vitabu vinavyosomwa mashuleni hawagusii hata kidogo kama vile ukombozi wa nchi ulipatikana. Kwa hivyo hizo holidays hata kama haziwezi kuongezwa moja yao ipinduliwe ndiyo iweze ku-suit hayo matakwa yetu.

Lingine sikusikia Katiba ikizungumzia vitu vya nchi hii kama vya zamani kuna vitu vya nchi hii kama vile vitu vya historical na sikuona mahali zimehusishwa kwa upande wowote ule. Kama buildings, kama vitu vyetu vinatokana na sisi. Kuna vitu vinatokana na sisi na vinatakikana viwe vya kitamaduni za kiafrika, values zake ziwe, sikuona mahali zimewekwa mkaso.

Kile kingine ni kuhusu mashamba, nimeona pia mnapendekeza kama vile tu mkoloni alikuwa anaweka lease ya 99 years. Sasa hiyo mmeweka ya 99 years na kwa sababu hiyo watu wa Kenya ni wengi na wanazidi kuongezeka ingepupishwa kusudi wewe unaondoka mwingine anapata na mambo ya nchi hii inakwenda mbele.

Kingine nikimaliza sikuona mahali mmetaja wale watu walipigania nchi hii na watu wale wengine wali-contribute nchi hii kwa njia ingine ile sikuona mahali ambapo wametiwa maana na sikuona mahali wamezungumziwa popote. Kwa hivyo vitu kama hizo zingefaa sana ziangaliwe kama zinaweza kuwekwa kwa katiba kwa sababu nafikiri watu walikuwa wamezungumzia. Asante.

**Serah Wambua:** Kwa majina ni Serah Wambua. Nataka kuongea juu ya administration. Mimi naonelea ni lazima kuwe na ma chiefs, assistant chiefs na wazee wa kijiji. Kwa sababu gani? Security ya area hizo iko juu sana na wazazi wale wazee sana hawawezi kufikia polisi kwa wakati ule wanapatwa na shinda. Lakini ikiwa assistant chief ako karibu, mzee wa kijiji, watasaidika haraka kuliko mtu kuenda kwa polisi.

Ya pili ni security ya polisi. Hatuna security kabisa hapa Kenya. Watu wako na shida sana. Mtu akifanya kosa anashtakiwa akienda polisi unamuona kesho anatembea. Usaidizi wetu uko wapi sasa? Sisi tunashidwa tunaelekea wapi kila mtu ako na usaidizi wa Mungu wakati huu lakini si wa polisi hawa wa Kenya.

Ya tatu ni upande wa akina mama. Akina mama wengi hapa Kenya wamekuwa come we stay. Come we stay ni kusema nini, unaweza kuolewa na mwanamme unazaa watoto zaidi ya kumi, tano na hajatoa hata dowry hata kidogo kwa wazazi wako. Hiyo ndiyo inaitwa come we stay. Hiyo sisi hatuoni ni vizuri. Kunatakina kuwe ukioa mwanamke wa mtu amezaliwa, hata nyinyi wanaume ndiyo mnazaa wasichana akimuoa atoe dowry ajue msichana wake ako kwa mtu. Sio kukaa mwishowe unakuja kumfukuza, umeweka bibi mwingine mahali na huyu umeaza kumtupa security inaingilia. Security ya boma sio nzuri. Wanaume wanatakikana kujua ukioa bibi umeoa bibi wa kukaa nyumbani yako. Akiwa na mtoto ama hana mtoto, kuzaa mtoto ni matendo ya Mungu si ya binadamu. Kwa hivyo mjue ukia na bibi inastahili umpe heshima yake ile inastahili kutosha hiyo ndiyo tunataka tupewe. Tupewe heshima ile inatakikana ile tuweze kukaa kwa boma ndiyo tuishi na raha

Ya nne ni upande wa mashamba. Kuna watu wamesema mashamba iko na acre nyingi sana, 99 years, hakuna mtu siku hizi ana 99 years, ni wachache sana watu wengi wako mbali. 99 years unapewe shamba ukae peke yako na watu elfu kumi hawana hata quater acre. We hii miaka 99 na uko na shamba ya elfu mia moja ya fanyia nini? Tunataka kila mtu awe na share ya kila mmoja at least awe kwake anakaa vizuri na si mtu mmoja awe akifaidika na wengine wanaomba omba huku barabarani. Hiyo hatutaki.

**Com. Abida:** Nyuma kabisa. Lakini msiseme maneno mingi ili kila mtu aongee.

**David M Kitika:** Jina naitwa David M. Kitika. Kwa upande wangu kwanza nirudishe shukurani kwa tume ile ilikuwa inaendesha hii kazi na ikafanya kazi nyingi kupitia wakati huu. Kwa hivyo vile naona ukubali usikubali neno Justice imepoteza dhamana yake hapa nchini. Kwa hivyo lazima tuangalie vile justice inaweza kuwa na maana kwa sababu imepoteza imani yake. Kwa hivyo kwa mfano kama ile alama imepewa polisi utumishi kwa wote utafaidhika sana ukiangalia hiyo maneno inasema. Ukienda polisi unaona majaabu. Kwa hivyo mimi ningesema lazima tufikirie, tuzikizane sisi tumekosea njia na kama vile ule

punda alipigwa na mtu mwingine alikuwa anaitwa Balaam na punda mpaka akalia akasema kama mtu lazima tukumbaliane sisi tumeenda against mahubiri ya Mungu isipokuwa mimi si muhubiri, lakini nafikiri tumeenda too much. Kwa hivyo sasa lazima tukubaliane sisi tubadilike na tukikubali kubadilika nchi hii yetu itakuwa safi sana. Asante sana.

**Authur Nzomo:** Asante, majina yangu ni Authur Nzomo. Zangu ni observations ambazo nafikiri tatu nne ambazo ningetaka kutaja. First we have the preamble. Nilikuwa nafikiria katika the preamble kwa sababu if you look at the draft now na politically imeanza kupigwa kila upande, katika ile wording vile we are exercising our sovereign and inevitable right, ile right nafikiri kwa maoni yangu tumeongezea ile neno inviable ili isije ikawa violated na mtu yeyote ule. Kabla sijatoka kwa preamble ningefikiria ingekuwa jambo la muhimu sana kungekuwa included the national motto. We place somewhere in the preamble the national motto.

Nafikiri itakuwa ya maana. Kisha nikitoka pale, ile ni kuhusu ile national days, kama mwingine hapa amesema nilikuwa na hilo wazo kuongezea katika ile siku tatu kwa kitaifa. Ingekuwa vizuri sana tukiongezea heroes day. Nafikiri hiyo ni ya maana sana katika historia yetu. Na kwa hivyo ingekuwa na maana sana ingeongezewa katika zile national days.

Chapter 6 that is dealing with the functions of the Electoral Commission. Hiyo ningependa munijibu sikuelewa vizuri tumeona kwamba among the functions of the Electoral Commission the settlement of electoral disputes, then what will be the position of the court concerning electoral disputes. Hiyo sikuelewe vizuri.

Halafu oni la mwisho ni kwamba the constitution should have a provision somewhere in the provisions on how the currency should look like. Ili isiwe ni ile shida ya tuko na Rais mpya anapindua sura ya pesa yetu note ama zile sarafu. Asanteni.

**Alice Kimweli Mutunge:** Madam Commissioner ni asante sana kwa kunipatia hii nafasi. Naitwa Alice Kimweli Mutunge. Nazungumza mambo matatu kwa uchache sana. Ya kwanza ni juu ya hizo National holidays. Kwa upande wangu nilikuwa naonelea kwamba ule mwanishilizi wa taifa la Kenya ambaye alipigana sana akaleta uhuru kwa Kenya ambaye ni Mzee Kenyatta nilikuwa nikifikiri ni vizuri atabuliwe kwa maaana kizazi kijazo kitakaposikia kwamba wako uhuru hawataweza kujua wamepata uhuru kutoka wapi. Kwa hivyo ni pendekezo langu kumtambua huyo mzee Kenyatta aliyepigania uhuru wa Kenya.

Jambo la pili ni juu ya administration. Kwa upande wangu mimi naonelea ya kwamba administration ingembaki na iwe inaandikwa na serikali hii ya security ya rural areas. Maana huko reserve kukiwekwa watu wa kuchaguliwa wengine watakuwa wanapendekeza, lakini administrator mwenyewe akiwa ameandikwa na serikali anaogopewa kure kijijini maana uhalifu umezidi kule na kunahitajika mtu ambaye ni administrator.

Jambo lingine ni juu ya freedom of movement and resident. Inasemekana kwamba everybody has a right to free movement lakini hapo ni swali, kupata passport na visa ya kutembea inakuwa ni ngumu sana na ningeuliza Madam Commissioner,

mnapoenda kurekebisha mngeongeza jambo kidogo pale mpange ni njia gani ya kurahishisha njia ile ya kupata passport na visa maana inasumbua sana. Yangu ni hayo tu Madam, asante sana na Mungu akubariki.

**James Mutuku Mutua:** Thankyou Madam Commissioner, my names are James Mutuku Mutua. I will try to be very brief and to the point. In reference to article 44, (i) Kenyans have been given a broad freedom especially freedom to worship. I would rather that freedom be limited to exclude wayward sects and religions at the risk of being maligned when I get out of here to mention the Mungiki sect.

Article 38, part (iii) under family we are required to give permission to anybody who is above 18 years to get married and to have a family. I have a proposal that allows us it also includes a person of 18 years of sound mind. Otherwise we may end up with a problem where we have families born by people who cannot adequately take care of that family.

Article 107, part (i), it deals with nomination of members of parliament by individual parties proportionately, 107 (i) where the 90 seats are mentioned. In my opinion those number of seats are too many not unless we want to reward sycophants. If we are going to have an allowance for nomination, currently we have been having 12 nominated members but if thy are going to represent special interest then the 12 in my opinion were still adequate in any case the people who have special interest still come from within areas where there are constituencies and MPs so they have a double representation in any case.

Article 171, the Prime Minister is appointed from the leader that is the majority in the parliament, then the cabinet will be nominated by the Prime Minister so that the president may appoint them. Since we have put in place the draft constitution, new checks and balances for the president so that he is not entirely above the law can be impeached. Let us give that President the powers to appoint all the cabinet and also the Prime Minister. As we speak now I think there is a case in court where the judges are challenging some part of the draft constitution which requires them to retire early and may be if the constitution is enacted then they be required to retire at the age of 65. I believe some of the judges which we have and whom we shall have are above reproach. Let them continue upto the age they are required to retire unless there is good reason to have their services terminated earlier as stated in article 197.

Article 217 and 218 deals with devolution of powers we are still not clear as members have mentioned on the functions of the village, locational and district councils. Maybe the draft constitution should include the elaborate explanation of their functions. When I read through I felt that people actually elect members in their village and the village councillors if I may use that word will nominate into the locational council but there seems to be a discontinuity between those two and the district council. Can a way be found so that those two councils do not have their members directly presenting the masses in the district council. Maybe that continuation should be seen.

This is now to the officers who are here whose office end by January 3rd if we do not have a new constitution, what happens

then? We also are of the opinion that any time after the 20th of this month parliament may be dissolved. Will you still have any reason to continue working, if what we are discussing now will not be discussed in the conference which comes 30 days from when we started this process?

Last but not least, I want to refer Madam Commissioner to a newspaper article which appeared in the first draft constitution guidelines were produced that was on the 22nd of September where it appears to like you are not party to the launch of the document which we are now discussing, maybe at the end of the day you can convince us to draft you (interjection, Com. Abida: Inaudible) May be I can finish the question I think if you explained to us not just me I want to know why it is written update and not apology.

**Com. Abida:** (inaudible)

**James Mutuku:** Thankyou Madam Commissioner, there may have been a reason why it was indicated that you were absent I am not saying that you disagreed totally with what we have here.

**Com. Abida:** Have I disagreed ....... (inaudible)

**James:** You see you maybe perfoming a duty because you are a Commissioner, not necessarily because you agreed.

**Com. Abida:** Inaudible........ there is launch and participation. I was not in the launch when .....camera to sign kama nimekuwa hapa leo... I wish you had asked me to participate in the process and I would tell you yes I did participate Yes I was here collecting the views of the people.

**James:** I think my question is answered. Thankyou.

**Com. Abida:** And that is propaganda.

**Peter Mutua:** Thankyou Commissioner. My names are Peter Mutua. First I wish to thankyou for the good work which you brought to Kenya. To start with I want to take a few issues starting with the 8th schedule. And I think majority of us have had to the schedule which concerns the administration and more so when it deals with the devolvement of the powers of this country and I would rather wish the local administration be retained more so the chiefs, their assistance and the elders because of this reason. (interjection: inaudible)

I would wish again this chiefs and their posts be retained simply because when we go to the local councils they are administering now the local people are much closer to the chiefs and the assistant chiefs when it comes to solving the local problems. So I

would wish the constitution would have a part in that with the DC and PCs I have no questions. But the chiefs and the assistants let them remain there.

In chapter 12 which deals with the natural resources and the environment, I would wish the Commissioners include what is called equity of resources because the biggest problem in Kenya is lack of equal distribution of resources and we know Kenya is rich in resources. So we can have a modality on how this resources can be equitably distributed it can do good to the Kenyans.

The other thing is about the land tenure system and much has been talked about. I wanted to talk about the lease period. The lease period stipulated in the current constitution is too much wide for the 999 years they are too big. So the Commissioners can look into it and see that this land tenure system is reduced. It can make Kenyans at least have a share of the land.

The other thing although it has been mentioned, I want to emphasis on the nomination of Members of Parliament. I think this constitution which you are trying to adopt it states clearly that the members of parliament who are not competent enough if those members who elected them in feel they are not performing can be recalled back and if all goes well they will be sent away by either the people who elected them. So it is my opinion that these nominated members be reduced because when they are many like the 90 of them they have no consent to anybody and neither will they be recalled if they don't perform and their numbers will be reduced and I wish they can go to 12 which we have currently is good.
I think those are the only points I wanted to express. Thankyou.

**Teresia Nduku:** Asante sana kwa siku ya leo jina langu naitwa Teresia Nduku na mimi nimekuja nichangie hii sheria ya akina mama. Shida moja naona kwa hiyo sheria inapitia wakati kwa upande wa Managers, Assistant chief na chiefs, mjue sisi akina mama kwingine tunaokolewa na hawa watu, kwa sababu ukienda wakati huu wanajua kuna katiba inaenda kupitishwa kuwe hakuna machief wameanza kuwa na magaidi sana. Wanaiba maana wanasema hakutakuwa na machief. Kwa hivyo wameanza uhalifu kwa hivyo iyo iangaliwe sana kwa sababu kuna akina mama hawana mabwana, mabwana zao wamekufa, hawana nani wa kuwatetea na huwa wanatetewa na hawa manager, ma assistant chief na chiefs. Kwa hivyo hiyo iangaliwe sana tusije tukapotea akina mama na watoto wetu. Kwa sababu ukiona mji una mzee unalinda boma yake ikiwa usiku anatoka ikiwa huyu mama hana nani wala nani. Kuna mama moja juzi tu niliona wakati mliweka sheria mnataka kupitisha ati mama akipigwa na bwana aende ashitaki na huyu mama alipigwa akaumizwa sana. Wakati alipona bwana ake akahakikisha hiyo kesi haitaendelea. Wakienda siku ya kesi anawahirisha kesi. Mama hana pesa, na inapelekwa Nairobi na yeye ako huko chini kabisa upande hii Mtito Andei na unajua hatuwezi kutoka huko kuenda upande hii. Mpaka mzee anamwambia nitakuhangaisha mpaka ukufe, kwani umwangalie sana kwa sababu kuna wengine mnaona mtu ameshtakiwa, amepiga bibi yake na amewekwa cell, kesho yake unaona mzee ametokea wanaenda wanamtoa. Kwa hivyo tunaona machozi tu kwa sheria zingine zikipitishwa watu wetu wataumia na watakwisha. Maana wengine hawajasoma, hawana chochote, hawajui judge ni nani, hawajui nani, na wako kule ni maskini tu na wanazaa maskini Kwa hivyo mimi ningeomba hii sheria tafadhali tusije tujitengenezee sheria yetu

itumalize, imalize watoto wetu na wajukuu wetu watakao kujua nyuma yetu. Kwa hivyo hiyo iangaliwe sana hata afadhali museme DO, DC, hao afadhali waondolewe lakini manager, assistant chief na chief ni watu wanafanya kazi kubwa sana. Maana ukipata na shida unapata kwake, unamuona mnaongea, mnajadiliana na anasaidia. Hata kama anachukia hachukii wote tena ingine mnasema atakuwa anachaguliwa na wananchi. Wewe ukinichagua ama nikikuchagua si utanihudumia mimi na yule amekukataa si utamkataa hata hivyo. Kwa hivyo hii sheria iangaliwe sana. **End of tape 2**.

....anatafuta tu njia yote ya kupata. Kwa hivyo akiwa na pesa, unaangaishwa na ukienda tu kwa makesi ya aina hiyo huyu hata hawezi kusikilizwa. Sijui mtaweka hiyo sheria iwe namna gani kwa maana hiyo ni shida kubwa sana kwa sababu ukishidana na mtu ana na anajua hii ni yako na wewe huna nguvu si atachukua? Kwa sababu huna chochote cha kujitetea, huna pesa za kujitetea na sheria zingine tuangalie.

Na hiyo sheria ya mashamba unaweza kutembea kutoka kule Mtito Andei mpaka kule upande wa Kisumu huko huko ukiona unaona mashamba mazuri tu, mashamba makubwa, unasikia watu wamepata shares wanafuga ng'ombe na hizo ngombe hazizaidii wao zinasaidia wale wakubwa maana sasa inaonekana ni kama ile watu wanasema wale samaki wakubwa ndiyo wanakula ile ndogo. Kwa hivyo ni kumalizwa tu na mashamba iko. Si watu wapewe wengine hata hawana pahali pa kujenga nyumba. Unaweza kuona nyumba moja inakaa watu kumi mzee na watoto wake kwa maana hakuna mashamba. Kwa hivyo tukitengeneza sheria tuangalie. Sisi Waafrika ni watu wa shida wakati wowote sio kama Wazungu wana pesa na kila kitu. Lakini sisi ni maskini. Hata hivyo wale maskini ndiyo wengi kuliko matajiri. Kwa hivyo hiyo naomba sana wakitengeneza sheria ingine waangalie sana na nitakoma hapo sitamaliza wakati. Asante sana.

**John Musyoki:** Kwa jina naitwa John Musyoki nataka kuchangia mambo matatu au nne. Kwanza nataka kusema tukiwa hapa siku ya leo ni lazima tutume wale watu tumechagua wakienda katika delegate mambo ya constitutional review waseme tunataka katiba mpya ifanye kazi. Kwa nini? Ile pesa imetolewa mingi juu ya kutengeneza katiba kama wananchi wa Kenya wangenjua itakuwa ni pesa ya kuharibu masaa hata kwetu wanakenya tunasitikiko kubwa sana. Kwa sababu saa hii naongea hiyo pesa ingefanya mambo ingine kama kulipa waalimu au kufanya kazi ingine kusaidia mwananchi wa Kenya.

Ya pili nataka kusema mambo ya election. Mambo ya kupiga kura tunapiga mwezi wa December na ingekuwa vizuri irudishwe nyuma kwa sababu mwezi wa December ni wakati wa Chrismas na kuko na mvua kwa hivyo ingeletwa mwezi wa nane au wa tisa.

Nikienda kumalizia tukiwa tuko hapa na tunatengeneza katiba ni lazima sheria ifuatwe, ikiwa tuko na Katiba ni lazima sheria ifuatwe. Kwa nini? Tukiwa tuko hapa na tunakuja hapa juu ya Katiba hatuwezi enda kado ya Katiba tutaenda kwa yale imetuleta hapa kwa hivyo ikiwa ni mwananchi wa Kenya apewe nafasi, wacha mambo ya chama, kama ni kuchagua, tuchague ule mtu anafaa na hiyo ipewe mwananchi afanye kupenda juu yake. Thankyou kwa hayo machache.

**Samuel Nguava:** Asante kwa kupewa hii nafasi. Jina langu ni Samuel Nguava. Ile ambayo nataka kuanzia nayo kuchangia ni water project. Sehemu hii yetu hatuna maofficer ambao wanaelezea juu ya maji maana tukiwa na maji mboga ambayo inatuchumbua sisi katika sehemu hii ya ukambani, nitasema namna hiyo, haitakuwa shida sana, tukipata maji ambayo ni hii inapita hapa nyingi zaidi mambo itakuwa ni sawa sawa.

Ya pili ni habari ya ajali barabarani. Hiyo imekuwa shida kubwa. Ukifungua radio sehemu zote za Kenya watu wanakufa kila dakika na kuna kitu ingine ambayo hata sijui tutafanya nini juu ya hiyo. Unasikia fulani amekufa ikiwa ni msichana, mwanamke, mwanaume wakatajwa majina yao. Na wengine huwa na pesa nyingi na hatujafikia hata kidogo pesa ikitanjwa, inakwenda wapi? Hiyo inaonekana kama kuna watu wanataka wengine waanguke na hiyo mitokaa wajitajirishe. Kwa nini pesa hazitajwi na majina yao na tunajua ni lazima uende mahali fulani ukanunue vitu au ukachukue pesa wana elfu kumi ama ni mia moja. Ikichukuliwa ni wale ambao wanakaa karibu na barabara kwa nini hawataji hiyo ndiyo ijulikane? Hiyo ni sawa sawa? Kwa nini haitajwi na tunajua watu wana pesa nyingi.

Ya mwisho ni medical department, kwa wakati huu serikali yetu haiijangii watu vile inafaa. Unaona mwanamke anabeba mtoto akiwa mgonjwa sana anakuja anaketi chini asubuhi mpaka saa ya njioni unamkuta hapo. Kwa nini hawezi kuchukuliwa ni taabu yake ikaonekana mara moja. Wale madaktari tulikuwa nao mbeleni sasa wako na hiyo ichunguzwe sana. Kwa hivyo yangu ni machache na iangaliwe sana.

**Joseph Kioko:** Asante Madam Commissioner, Kwa jina naitwa Joseph Kioko. Nitaongea juu ya mambo inayohusu vijiji ama area ambazo kama sasa tuko kwa sababu hata constitution iwe namna gani ikiwa haitatui maneno ya raia wale wa chini haitakuwa ya maana. Kwa hivyo ningetaka kuongea juu ya national resources na kupendekeza ya kwamba pesa kiasi fulani kipelekwe katika kijiji au sub-location ili ingine ibaki Nairobi halafu ikutanie mahali. Na pia nipendekeze katika kila wilaya kuwe na development bank kwa sababu hawa raia kama wa sehemu hii hawana pesa mahali na iwe na projects katika locations ambazo ni za kuleta pesa karibu na wananchi. Pia ningeuliza, jua kali industries zitolewe Nairobi ziletwe katika local centres, markets n.k. kwa sababu mwelekeo sasa industries zote ziko katika towns kubwa na zinahitaji kupelekwa katika rural areas.

Pia ningependekeza mambo ya medical katika kila village kuwe na daktari ama katika kila health centre ambaye ameajiriwa na serikali na anahudumia watu. Kwa sababu university kila mwaka zinatoa graduates wa medical na hawasaidii wananchi.

Ile ingine ningesema serikali itafute njia ya kufanya uchunguzi kwa sababu sehemu kama hii tuliko more than 50% kuna mawe hakuna kitu kingine na kama italeta njia ya kutengeneza kama kogoto industries akina mama na nini watasaidika. Kwa hivyo nitafika hapo.

**Japheth Ndeto:** Jina langu ni Japheth Ndeto na yangu ni mawili tu No.44 inazungumza juu ya freedom of religion, belief and opinion. Vile nimeona na vile nimesikia hapa Kenya watoto wamekuwa wakipotea sana na inasemekana kwamba dini zingine

zina imani chafu ambayo kwa ibada zao wanatoa sadaka za watoto. Ningeuliza hii constitution yetu mpya ichunguze dini, iangalie kile wanaabundu, vile wanaabundu na zile zinaumiza watoto wetu wandogo na hata wale wengine hawana akili timamu zifutiliwe ziwe haziko Kenya

Kwa vile civil servants wanalipwa mshahara wa chini sana ningeuliza ile voluntary retirement age iwe reduced to 20 years ikiwezekana. Asante. (interjection: inaudible) Nasema after 20 years of service. Thankyou.

**Obadiah Muteti:** Asante sana Madam Commissioner, na ma-officer wengine wa Commission. Kwangu narudisha shukurani zangu kwa Commission, wakati ule mwingine tulika hapa tukipatiana maoni mengi ya hiyo niliyatoa nimesikia yametanjwa leo na ni asante kwa uchunguzi wenu wa yale makaratasi.

Hata leo ninamengine lakini nitashika moja hapa na pale na nitaiacha ichunguliwe. Jina langu ni Obadiah Muteti.

Katika Preamble katika hii draft imeleta hakuna mwanzilishi wa taifa hii letu na tukiangalia taifa kama America wanamtaja Washington, huko Uingereza pia vile taifa ilianza tunaona hii ni ya maana tuweke kiongozi wetu wa taifa alieanza hii. Na pia historia ndogo vile wakati ya ukoloni ilikuwa na vile tulipata uhuru na vile katiba ya kwanza ilivyoanza na hii ndiyo mara ya pili tunaingilia Katiba iwe kidogo inaonyesha.

Ile ingine ningesitisha ni hiyo Heroe’s day (Kenyatta day) iwe ndiyo yetu ya kusherekea Heroe’s day na watu wa uhuru struggle wanasema iwe ndiyo siku tunakumbuka hiyo group.

Katika zile directive principles of state policy wakenya wote wanahitajika ku-participate kwa kutoa kodi wengine hawatoi kuna wengine tunaona kuna ng’ombe nyingi lakini wakienda kwa maduka wanafinya kila siku na hawa watu wa county councils wanataka kodi nini hata kiosk huko nyuma haitolewi kodi na kuna watu wengi walio na mali sana. Kwa hivyo taxing is not proportional. It should be considered. Thankyou.

Then tunaangalia kuna watu wengine ambao ni wazee sana na wakiingia katika uzee hawangaliwi masilahi yao. Katika Kenya yetu tungetaka wale wanakuwa wazee sana wawe wanapata kitu kidogo kutoka kwa serikali. Huenda ikawa hakupata kazi ya kumpatia pension lakini imefikia pahali wanataka kitu ya kula hapatiwi kitu.

Consitutional supremacy, nafikiri hakuna part of this constitution ambayo inataka kufanya rekebisho mbila wananchi kuulizwa. Hata ikiwa mnataka ipelekwe parliament ifanye, kwanza wananchi waulizwe which part inaweza kupinduliwa na parliament, tupatie parliament right ya kuenda kupindua. Kwa kuwa wakati mwingine parliament fulani inawezaa kaa chini na ikafikiri tupindue to suit sisi. Lakini tunaona ni heri itoke kwa hawa watu.

Political parties – hizi parties ziwe kama nne hivi, zikiwa nyingi zinaharibu mafikira ya watu. Wengine watakufa wakiwa confused kwa hivyo nataka nchi yetu ipatiwe proper guidance as to why we are on these political areas of thinking.

Structures and systems of government. Regional government ile tunasema majimbo kwa wakati huu tungengojea mpaka ipite miaka 50 hivi ama a 100 ndiyo watu wawe kila area ina mali ya kutosha (interjection: Com. Abida:..... (inaudible) unaona kama kuna majimbo) Hapana mimi nasema (interjection: inaudible) My point was coming next that is the present provinces we have we need to have fair distribution of National institution like the universities, teachers training colleges, technical colleges and also factories. If we think of the sand bricks which are made at Nairobi they should be make in a place where the sand is plenty. We have these juices, jams zinatengeneza Nairobi na haja tunapeleka hapo mbooni ama Kisii ama pahali ingine ndiyo hiyo factory I-employ watu kwa kazi huko reserve. That is the major point I was coming to.

Then on natural resources we have water running down our rivers and just the land next people are suffering of hunger we would request that the constitution to enlight our government that this water can be diverted to adjusten land for irrigation. (interjection)

**Com. Abida**: What I would suggest please don’t give me views, give me comments that relate to draft constitution..... (inaudible)

**Obadiah Muteti:** We were told by teachers to hand in more points when we come this time. Then on today because I have a paper on that there is a place you mentioned on children being cared for but there are children who become very strange at homes and they even overpower the parents. I think the present constitution should set law where these children are also reported to the government by the parents and they are put in a juvinile school where they are corrected. We have the chokoras in Nairobi who have just run there and they come from well-of families.

Two when children go to school in our state I think they should be educated coming up with principles of skill which would help them. For example when they are in standard one we see they are able to learn some driving and building so that as they come to the university they have come to know those skills in advance stage so that our people are not handicapped with knowledge.

On arrest you mentioned of our keeping quiet until we speak in court but I was feeling that when I am arrested I should keep quiet but before that the officer moves me to the custody he should explain to me I have arrested you because of such and such a crime, so that I know clearly where I am so that when I know clearly I may be pushed until it is too late to understand why I am pushed. The psychological effect of thinking can confuse me.

On ethnic groups we have about 42 tribes in our country and we think that they can form our nominated members for whatever law is made in National Assembly as a senate of this 42 I think it is worthy it to have it through.

Women representation in my view I think it should be reduced to 20%. Of the leaders in the village that person who comes to head the six wazee should be taken to a civic training for a week or two and he should be paid because he handles the most serious cases.

International laws – there are some laws we go to sign with those other nations and when we come back here you find that they have ousted our laws. For example today we have a law saying we should not beat children at school as punishment and the secondary school children have become very arrogant teachers are not able to teach them and this has brought down the good discipline of our secondary school children. I think when a law is made in international agreement before it is enforced in our state let the parliament seat and see whether it will suit and promote our country the way it ought to.

When we come to the voting we find that we have 50,000 registered voters and only a third went to vote where have the other twenty gone? I think the Electoral Commission should look into this one to prove where each one went because that is a person who should have his decision made. After all he is a person who comes to say we don't want this person we didn't elect him they did't go to election, infact they break the law by not voting on the voting day. Thankyou Madam and your officers.

**Com. Abida:** Please be brief otherwise I may have to close the session .... (inaudible) don't repeat and don't tell irrelevant things.

**Monicah Mutua:** Asante. Jina langu naitwa Monicah Mutua. Point yangu ni moja. Sijasikia vizuri lile tuliongea juu ya orphans ijapokuwa hii Katiba ni sisi tulitengeneza lakin saa ingine unatengeneza kitu unaona kinaharibika mahali unatengeneza tena. Sikusikia vizuri vile tuliongea juu ya orphans (interjection: inaudible) tulisoma kwa hii lakini hatukujua vile watafanya mimi naonelea kwa maoni yangu iwekwe kwa katiba iwe division iwe na a cortage mahali hawa watoto wakiwekwa pahali pao mbila mtu wa kuangalia hata mmoja wawe wanapelekwa huko wakaishi huko na wale wa kukusanya wawe ni machiefs na assistant chiefs, wawe na kazi hiyo Asante.

**Joseph Kiko:** Kwa majina naitwa Joseph Kiko, na ninataka kuchangia mambo mawili au matatu. Moja ni reference ya Bill of Rights article 38 ambayo ni ya familia, ningeonelea kwamba registration ya property iwe ya mama na bwana ambao wako kwa familia kwa sababu wakati mwingine mabwana wakifa wanawacha hiyo mali kama property ya bwana huwa inanyanya ule mama ambaye amebakia. Na kama wametafuta hiyo mali pamoja ingekuwa vizuri hiyo mali ingeandikishwa wote wawili.

On the security issue, tuliseme maneno ya polisi na nikashangaa wakati mama amepoteza ng'ombe na anakimbia kwa polisi anakuta labda polisi haina mafuta na hiyo ng'ombe imetolewa sokoni. Kwa hivyo naonelea security ya mambo ya mali ya wananchi haikui vizuri sana vile itakuwa inachungwa.

Ya mwisho ni kuhusu land matters katika hii sheria ya constitution tumekuwa na Cap 284 laws of Kenya nilikuwa na hii tribunal courts lakini ningeonelea kulikuwa na locational tribunal court ambayo itakuwa ni indeginous ambao members watakuwa ni wale wale ya hiyo area na hao ndiyo watakuwa wanaweza kutekeleza maneno ya mashamba katika area Asante sana.

**Phillip Ginda:** Jina Phillip Ginda. Swali yangu ni hii sisi wanakenya kitambulisho yangu inaandikwa Mwanakenya na mimi ni Mkamba, kuna Mkikuyu na hii na hii, sisi wote tunafuata njia moja maana mimi ni munyonge, ule ana nguvu na utamaduni wetu sisi Wakamba tuna utamaduni, huyu mwenye nguvu ana kuja anaingiliana na wengine wenye nguvu sasa wanakuja kuninyang' anya mali yangu. Sasa nikipita kwa huyu ninapinduliwa hapa, nikipinduliwa hapa, na pinduliwa pale mali yangu inapotea, sasa utamaduni wa katiba hii ni gani. Kama sisi Wakamba tulikuwa na kitu kinaitwa githitu. Kama wewe unakibizana na mimi namna hiyo na mimi nitapigia wewe githitu, na wewe mtaanza kufa moja kwa moja hiyo ni utamaduni wetu.

Hiyo sikuisikia kwa Katiba. Ile ingine swali ingine ya pili ni hii, mimi nimezaa watoto wake na wanaume, sasa msichana tayari ameshaolewa, nikaletewa mbuzi mbili utamaduni wetu, anarudi hapo sasa katika ile shamba yangu, nitagawiya yeye?

Hiyo ni ingine. Katika Katiba maana hii Katiba tulianzilia kwa vitu tatu ile tulipigania uhuru, mimi nilikuwa moja wao na ile kitu ni tatu, umaskini, kutojua kusoma, na ugonjwa. Tuseme kutojua kusoma kumeendelea isipokuwa kuna shida shida hapo ndani ya pesa, lakini ugonjwa unaleta taabu, mimi ni munyonge, sijui mahali naweza pata shillingi tano, mimi naungua, nikienda hospitalini mimi naambiwa leta hapa kumi, pale ishirini, pale thelathini sasa nitatoa wapi. Kwa hivyo ile katiba tunataka kuitengeza vile ilikuwa mwanzo tulipopata uhuru na Mzee Kenyatta magonjwa watu wanatibiwa, nendeni mkafanye kazi, maana ni Uhuru na kazi, nendeni mkafanye kazi maana mmepona. Hiyo kupona ndiyo unamaliza umasikini maana ukiwa mgonjwa huwezi fanya kitu.

Elimu ilikuwa inapeanwa bure sasa ile pesa na tulikuwa bado wachanga tulikuwa hatuna kitu ilienda wapi. Kama imeenda na hii Katiba iko na hii Katiba iondolewe sababu ile maneno inasemekana tunataka Katiba ile ya zamani iendelee. Mimi mwananchi wa Kenya sitaki hiyo Katiba, Katiba ile tunataka iendelee kwa serikali mpya ni Katiba mpya serikali mpya, mimi nasema hivyo. Mimi nafika hapo.

**Raphael Kituku:** Asante sana Commissioner jina langu naitwa Raphael Kituku. Ninaongea sana juu ya hawa wazee wa kijiji, wazee wa ukoo. Hawa wazee wa ukoo baada ya ile government ningeonelea hawa wazee wa uko wapewe nguvu zaidi. Kwa hivyo hawa wazee ikiwa wanatumia haki wanafanya kazi yao vizuri hii mambo ya mashamba yote wanajua mipaka ya ukoo wao. Ni bora kusema ukweli. Mizozo ya familia wanajua kila kitu ya uko wao wanajua chanzo na kama nasema ukweli wanatoa hiyo mizozo watamaliza.

Ile ingine ni juu ya chokora. Hawa watoto ni wetu na wanazidi kuongezeka. Mimi nikiwa mzazi, wewe yule mwingine tujaribu

sana nchi yetu ya Kenya tupunguze hawa watoto kuingia mijini. Ukienda hapa nchi saa hii wameanza kuingia, karibu kila soko nchini Kenya wameshaa ingia na baadaye watakuja kuwa gang ama watаunda serikali yao. Kwa hivyo hiyo jambo iangaliwe.

Ya mwisho ni habari ya maji. Nikisema maji mvua inanyesha sana hapa Kenya lakini baada ya siku tatu, nne siku moja hapa kwetu ukambani utakuta maji hakuna. Ningeonelea kama serikali inataka kutupatia maji ya kutosha na safi kwanza ituchimbie silanga ama mabohole ya maji maana ikisha chimbwa hiyo ni tupu mvua ikinyesha maji inaingia pale hakuna mvua inatumia huko hakuna watchman wala nini. Kwa hivyo hiyo tunjengewe madam ya kutosha halafu baadaye wanakuja piping baadaye. Asante.

**Com. Abida:** Asanteni kwa maswali yenu nitajaribu kuyajibu kwa kiwango niwezacho na swali la kwanza lilikuwa la Jonathan Muoki kuhusu elimu ya ufundi na elimu ya ukulima. Kwanza kabisa ningetaka kusema Katiba haiwezi kuandika mambo yote ambayo tungetaka kuyaona kwa sababu katiba ni muongozo wa utawala. Kwa hivyo kuna mambo ambayo yatakuwa yamesemekana kwa juu juu na mengine yamefichika lakini tuna sheria ambazo zina fuata sheria hii kuu ambazo huwa ina sheria ambazo zina sema mambo mengi zaidi lakini kuhusu elimu ya ufundi ningemuoba Bw. Jonathan Muoki aangalie article 58 subsection 3 ambayo imesisitiza elimu ambayo ni elimu kupitia au zaidi ya shule ya upili. Nafikiri elimu hiyo itakuwa iko covered pale kwa sababu hatukuweza kuandika mambo mengi zaidi.

Halafu katika education ya agriculture, ukiangalia article 15 (e) tumesisitiza kwamba ni jukumu la mwananchi kuweza kujifundisha zaidi ili kuweza kuinua hali yake ya kimaisha kwa hivyo nadhania hapo pia tumecover pengine tungesema ni kwamba hiyo ni jukumu la serikali kupatia wananchi hiyo elimu lakini tumesema kwamba wananchi wajihimishe na wajaribu kusoma zaidi.

David Kimuli alizungumzia kuhusu mizozo ya mashamba na angependa tuwe na mipaka ambayo ilikuweko wakati wa ukoloni, mambo hayo tuliyasikia tulipokuwa hapa na kwa sababu kuna mambo mengi ambayo hatukuweza kuiandika katika Katiba na pia hatukuweza kuyashululisha kwa sababu hatukuwa na muda wa kutosha wa kuweza kufanya upelelezi na kujua mipaka hiyo ya ukoloni ni ipi sijui kama wananchi wote wangependelea, tumependekeza kuwe na tume ya mashamba ambayo yatashuluhisha mambo kama haya. Kazi yake iwe ni kutatua mambo kama hii ili kuweza kutatua mambo ya mashamba na tumependekeza kwamba serikali itatue mambo kufikia miaka miwili baada ya kupitishwa kwa hii Katiba mpya.

Kulikuwa na Mzee jina lake la kwanza ni John sikupata la pili ambaye amesema sikuzungumzia kuhusu Ministry of Information. Hatukuweza kupendekeza wizara za serikali. Nafikiri tulidhania ni jukumu la serikali kujua wizara zinazotakikana katika nchi kwa sababu tukiandika katika katiba iwe wizara fulani kazi yake sio muhimu itamaanisha kubadilisha tena na tumeachia hiyo kazi baraza la mawaziri na waziri mkuu lakini ukiangalia pia tumependekeza kwamba katika article 47 kwamba iwe ni haki ya kila mwananchi kupata habari kutoka kwa serikali. Kwa hivyo inakuwa ni jukumu la serikali kuweza kupitia kwa wizara ama kupitia njia nyingine kuweza kukuletea habari.

Na kuhusu hizi nakala za mswaada huu wa Katiba kama nilivyo waelezea tena kwa sababu ya muda nyinyi hapa wengi wenu mmesema au mngetaka Katiba haraka iwezekanvyo. Hatukuweza kuketi Nairobi tukisisubiri lakini kupitia juzi zilikuwa zimetoka na nafikiria Bwana Coordinator anatumia wale Committee Members kuwafikishia hizo nakala za Kiswahili na kwa wale ambao walisoma Taifa leo hizi zilikuwa katika Taifa Leo. Lakini kwa vile tumezichapisha kwa niaba ya wananchi tutahakikisha zimewafikia hata ikiwa si kila mtu atapata lakini sitafika katika Constituency na sehemu bali bali kufikia wanakamati. Ikiwa hamkuzipata pia mtatafuta Bw. Coordinator katika ofisi yake kuweza kujua kama zimepeanwa ama ziko katika ofisi yake.

Na pia ukasema kwamba sikuzungumza kuhusu transport na insurance. Kama nilivyosema mambo yote haiwezi kuwa katika Katiba, kuna sheria ambayo inahusika na mambo ya insurance na kama sheria hiyo ni kinyume cha Katiba tumependekeza kwamba kwa miaka miwili ijayo njia zote tena ziwe zina andamana nakufuatana na Katiba yetu. Kwa hivyo hiyo sheria iko pengine inaweza kuwa sio kamilifu lakini iko.

Na pia ukazungumza upigaji kura na kwamba wannchi wasiambiwe wampigie kura mtu fulani. Katika hii Katiba yetu tumependekeza kwamba kila mwananchi awe na uhuru wa kumpigia kura atakaye. Na ukapendekeza kuwa kungekuwa na vyama via kisiasa mbili ama vitatu. Kwa hakika mambo haya tuliambiwa sana na wananchi lakini kumbuka pia mlituambia kwamba wananchi wawe na uhuru wa kuasiliana na kuandamana. Freedom of association. Tulipoketi katika mjadala wa Tume kabla hatujaandika pendekezo hilo tulijiuliza je, unaweza kuwa na freedom of association halafu uambie watu wasiunde vyama vingi vya kisiasa. Tukasema hapo kutakuwa na contradiction natukaonelea, pengine maoni yetu hayafai kwamba ikiwa vyama vya kisiasa vitafuata mwongozo unaotakikana na Katiba inaweza ikawa hatukuwa na vyama vingi kama tulivyonavyo wakati huu kwa sababu kuna vyama vingi ambavyo havitaweza kufuata msimamo huo wa Katiba na kwa sababu ya hiyo freedom of association ikawa ni vigumu sisi kuwaambia nyinyi muwe na freeom of association na halafu muwe na vyama viwili. Sasa kukawa na contradition na tukasema tuiwache hivyo lakini ikiwa mnaona kuna haja kubwa mtawatuma waakilishi wenu katika National Conference jambo hili liweze kujadiliwa katika confernce hiyo au kikao cha kitaifa kwa sababu sisi tuliona ugumu wa kuzuia political parties.

Na ukatoa pia pendekezo kuhusu corruption, na ukashidwa tutafanya aje kuondoa corruption na ukatoa mfano wa kortini na ukapendekeza kwamba tume ya mahakama iwe inatangaza malipo ya kortini. Sasa jambo la ajabu mimi nikiangalia ni kwamba ukienda kwa karani wa kortini na akikuitisha pesa si unatakiwa kuwa na receipt na ikiwa hukupata reciept hiyo ni wazi unahonga. Na ikiwa unahonga wewe uko na hatia kama mwananchi ikiwa sisi kama wananchi hatuachi kuhonga sioni kama tutamaliza rushwa katika nchi na ukiangalia article ya kumi na tano tumependekeza kwamba ni jukumu la kila mwananchi kuweza kutohonga na kumaliza hii culture ya uhongaji katika nchi yetu. Kwa hivyo nadhania ni jambo ambalo unashuruhisha wewe mwenyewe, ukienda kortini unapewe reciept na pengine hili ni jambo la maana sana unasema kwamba korti itangaze charges zake ili kila mwananchi ajue. Lakini pia ukienda kwa korti na uulize utaambiwa. Sidhanii ni sili, mzee pengine ni wewe

mwenyewe umekuwa mdhaifu kidogo.

Bw. Justus Levi alitaka nifafanue maana ya government na akasema kwamba tunatumia hilo neno kivibaya. Pengine hayo ni maoni yako bw. Lavi na ni mpaka tuyakubali unasema hata local government hatungeita govt. Lakini what is in a name. Wazungu wenyewe huwa wanapatia majina maana fulani wengine wakaauliza what in a name. Ikiwa village council itaitwa villge govt., Na itekeleze hilo ni neno tu lakini haijaharibu utawala. Lakini ungekuwa na pendekeza tusiite village government ingekuwa ni bora zaidi hii draft na tunaweza kuwa ni kosa. That is what we are calling it village council lakini it is a level of governance so that is why, in other words you can call it a government. It is a matter of usage of language. Lakini katika hii draft constitution we have named them village councils but in my interpretation is that you can also call it a village government. Kwa hivyo it is a matter of language which we can debate in the National Conference please send your representative and others so that we can use an appropriate word.

Na jambo lingine utakuta kwamba we have defined the national government. We have defined the executive and we have said who are going to be members of that executive, it is all there na kama nilivyosema ikiwa wengi wanafikiria tusisiite government tafadhali mpendekeze kupitia kwa MP na representative tuweze kubadilisha mambo haya katika the National Conference kwa sababu nafikiri watu wengi wakikutana wakiwa delegates 629 itakuwa ni bongo nyingi kuliko watu 29 na mambo pale pengine hayataharibika sana.

Pia ukasema article 171 inazungumzia kuteuliwa kwa waziri mkuu na hatukusema atateuliwa vipi na tungekuomba usome article 175 it is all there. Na article 162 ukasema inapendelea Rais. Sasa ubaya haukunieleza unataka kuona nini pale na mimi nikiisoma article 162 removal of president on ground of incapacity. Sioni kama kuna mapendeleo lakini ni mapendekezo ambayo yatatuweshesha kumuondoa rais ambaye hawezi tumikia nchi yetu. Again if you have recommendations you can pass them to your representative.

Na pia ukapendekeza kwamba Rais atolewe kupitia public referendum nafikiri jambo ambalo tulipendelea ni kwamba tukiwa na bunge la watu ambao wamechaguliwa kwa kura za haki na za harali watakuwa ni watu ambao wanatuakilisha kule na watakuwa ni watu tumewapatia majukumu yakuweza kufanya mambo fulani kwa niaba yetu kwa sababu nilizungumza about decisions being made by the public, every other day tutakuwa na kuwapa kazi mawakilishi wetu katika Bunge na pengine pia itakuw ni gharama ya juu ambayo pengine serikali haitaweza kutumikia.

